


# Uchoraji Shirikishi wa Ramani ya Rasilimali za Nyanda za Malisho nchini Tanzania

Mwongozo wa Uwandani wa kusaidia Kupanga Mpango na Usimamizi wa Nyanda za Malisho ikiwemo Kupanga Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi ya Kijiji

care

Jumuiko la Maliasili Tanzania

Tanzania Natural Resource Forum

ILRI

IFAD

Investing in rural people

INTERNATIONAL LAND COALITION

AFRICA / AFRIQUE

Maudhui ya kazi hii ni huru kutolewa tena, kutafsiriwa, na kusambazwa ili mradi taarifa imetolewa kwa International Land Coalition, na mwandishi wa makala na asasi. Isipokuwa kama itaelezwa vinginevyo, kazi hii isitumike kwa madhumuni ya kibiashara. Kwa taarifa zaidi, tafadhali wasiliana na info@landcoalition.org au fungua http://creativecommons.org/licenses/by-nc/3.0 Imesanifiwa na Federico Pinci. Picha zimechorwa na Aldo di Domenico. Kimechapwa kwenye karatasi zilizofanyiwa ujadidifu/FSC.

ISBN: 978-92-95105-24-9

# Uchoraji Shirikishi wa Ramani ya Rasilimali ya Nyanda za Malisho Nchini Tanzania

Mwongozo wa Uwandani wa kusaidia Kupanga Mpango na Usimamizi wa Nyanda za Malisho ikiwemo kupanga Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi ya Kijiji

Januari, 2016

# Shukrani

Miongozo hii kuhusu uchoraji shirikishi wa ramani ya rasilimali za nyanda za malisho imeandaliwa na Mradi Endelevu wa Usimamizi wa Nyanda za Malisho ('SRMP') nchini Tanzania[1]. Mradi ulibainishwa na kuandaa uchoraji shirikishi wa ramani ya nyanda za malisho kama zana inayotambuliwa kwa ajili ya kuboresha kupanga mipango na usimamizi wa nyanda za malisho ikiwa ni pamoja na kupanga mpango wa matumizi bora ya ardhi ya kijiji.

Mradi unadhamiria kuwezesha upatikanaji wa ardhi na haki ya rasilimali kwa wafugaji, wakulima-wafugaji na wakulima wa mazao nchini Tanzania wakati ukiboresha usimamizi wa ardhi. Mrad i umefanyiamajaribio ya kupanga mpango ya matumizi bora ya ardhi ya kijiji na wilaya na usimamizi wa nyanda za malisho katika wilaya za Kiteto, Bahi, Chamwino, Chemba na Kondoa. Mradi ulipata msaada wa kifedha na kitaalamu kutoka Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo (IFAD) na Muungano wa Kimataifa wa Ardhi (kutoka Mfuko wa Belgium wa Usalama wa Chakula), unaotekelezwa kupitia CARE Tanzania na Jumuiko la Maliasili Tanzania ('TNRF'); pamoja na wabia muhimu wakiwemo Halmashauri za Wilaya tano, Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi), Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi; Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi; na asasi za kiraia zinazosaidia undaaji wa mpango wa matumizi bora ya ardhi ya vijiji na usimamizi wa nyanda za malisho ambazo ni Programu ya Maendeleo ya KINNAPA, Mtandao wa Mazingira wa Dodoma (DONET), Mtandao wa Mazingira wa Bahi (BAENET ), na Mtandao wa Mazingira Chamwino (MMC).

1 Imetoholewa kutoka Miongozo ya Uchoraji Ramani katika Usimamizi Shirikishi wa Ardhi ya Malisho nchini Ethiopia na Ben Irwin, Adrian Cullis na Fiona Flintan (2014).

Kikundi kilianzishwa mwaka 2010 na Adrian Cullis na Ben Irwin, katika kushughulikia upoteaji wa haraka wa maeneo ya malisho na rasilimali za nyanda za malisho na athari mbaya sana zilizokuwepo katika mifumo jumuishi ya Usimamizi wa Maliasili na hususani katika mifumo ya uzalishaji wa mifugo. Lengo kuu la Kikundi cha Maeneo ya malisho ya Siku Zijazo ni kupambana na upotevu wa rasilimali za eneo la malisho kupitia masuluhisho na mikabala ya usimamizi wa kiubunifu na kiutendaji wa rasilimali za maeneo ya malisho. Mikabala hiyo inazingatia uandaaji wa matumizi shirikishi ya ardhi na mbinu za kupanga na usimamizi wa mipango ya maliasili.

Kazi za ugani na uzoefu zinazounda na kuelezwa katika miongozo hii zisingewezekana bila ya ridhaa, msaada na bidii ya jamii za wenyeji wafugaji, wawakilishi wa serikali na wafanyakazi wa Asasi sizizo za Serikali(AZISE) wanaofanya kazi kwenye maeneo ya wafugaji. Mwongozo huu unakusudia kupata na kuakisi maarifa, uzoefu na maoni ambayo watendaji wote hao wameyatoa katika mwongozo huu.

# Utangulizi

Eneo la Tanzania bara lina ukubwa wa hekari milioni 94.5 lenye matumizi mbalimbali ya ardhi ikiwa ni pamoja na makazi ya binadamu, miundombinu, kilimo, ufugaji na eneo la kuchungia, misitu, wanyamapori, uchimbaji wa madini n.k. Takwimu za hivi karibuni (2012) zinaonyesha kwamba nchi ina takribani ng'ombe milioni 22.8, mbuzi milioni 15.5, na kondoo milioni 6.9, ambao wanafikia idadi ya jumla ya Mifugo milioni 28.8 kwa mifugo yote . Hii inahitaji wastani wa hekta 2 za ardhi ya kulishia kila mwaka kwa kila mfugo mmoja, ikiwa inahitajika jumla ya hekta milioni 57.6, ambayo ni wastani wa asilimia 64 ya ardhi yote ya Tanzania Bara. Maeneo mengi ya ardhi ya malisho yameingizwa katika ufugaji na mfumo wa kilimo cha ufugaji kama nyanda za malisho.

Kupanga Mipango ya matumizi bora ya ardhi katika nyanda za malisho ina changamoto kubwa. Nyanda hizi zina watumiaji wengi na matumizi mengi ya ardhi na rasilimali, ambayo yanasababisha ugumu katika kupatikana, na taratibu za usimamizi na utawala wake. Mara nyingi mgawanyo wa rasilimali hubadilika na hautabiriki. Hii inahitaji uwezekano wa kukubali mabadiliko ya matumizi makubwa na ya muda mfupi, pamoja na kutozuiliwa kwa uhamaji katika eneo la nyanda za malisho. Kupanga na kusimamia matumizi hayo lazima kuzingatie na kufanyie kazi utata huo, badala ya kujaribu kurahisisha. Matumizi ya rasilimali yanayoshirikisha zaidi ya kijiji kimoja yanawezekana kuhitajika na kwa mujibu wa sera na sheria za Tanzania zinaweza kurasimishwa kupitia mipango na makubaliano ya pamoja na 'mpango wa usimamizi wa sekta ya maliasili' kwa rasilimali zinazotumika kwa kushirikiana.

Uchoraji shirikishi wa ramani ya rasilimali za nyanda za malisho, kama ulivyofafanuliwa katika mwongozo huu, ni zana muhimu kutumika katika mchakato wa kuandaa mpango wa matumizi ya ardhi ya kijiji katika vijiji vya wafugaji na wakulima wafugaji. Uchoraji huu shirikishi unaboresha uelewa wa matumizi, usimamizi na upataji wa rasilimali ya nyanda za malisho na kutatua utata uliofafanuliwa hapo juu. Uchoraji wa ramani sio kwamba unatoa taarifa za kutosha tu kwa kipindi cha muda mfupi, bali pia unaanzisha mchakato ambao unaboresha ushiriki wa wafugaji na wakulima wafugaji katika kufanya maamuzi ya kupanga mpango wa matumizi ya ardhi kijijini. Hali hii inachangia katika kujisikia vizuri katika umiliki miongoni mwa watumiaji wa ardhi ya nyanda za malisho dhidi ya mchakato wa kupanga mpango ya matumizi bora ya ardhi ya kijiji , na matokeo yake kuboresha motisha ya kuwekeza katika utekelezaji wa mipango hiyo, na uwezekano wa kupunguza migogoro ya matumizi ya ardhi.

Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi inapendekeza kutumia Mwongozo huu na uchoraji shirikishi wa ramani ya rasilimali za nyanda za malisho katika mchakato wa kuandaa mipango wa matumizi ya ardhi ya vijiji kwa maeneo yote ya wafugaji na wakulima wafugaji.

*Dr Stephen J. Nindi*
Kaimu Mkurugenzi Mkuu,
Tume ya Taifa ya Mipango ya
Matumizi Bora ya Ardhi, Tanzania

# Usuli

Mifugo ni sehemu muhimu katika uchumi wa vijijini nchini Tanzania. Mifugo si kwamba hutoa nyama na maziwa, lakini pia hutoa ngozi, nguvu kazi na mbolea. Mifugo inatoa mchango muhimu katika bidhaa zinazouzwa nje na Pato Ghafi la Taifa la Tanzania. Mifugo inashika nafasi ya pili ndani ya sekta ya kilimo katika kuchangia Pato Ghafi la Taifa (hii ni karibia asilimia 13 ya Pato Ghafi la Kilimo la Taifa). Hiki ni kiwango kidogo licha ya kuwa na idadi kubwa ya mifugo. Hii inasemekana ni kutokana na kuwepo kwa magonjwa, ambayo yamekuwa kikwazo kwa usafirishaji wa wanyama nje ya nchi. Sekta hii pia inakabiliwa na matatizo ya kutoendana na mahitaji ya soko jipya kama vile Mfumo wa Ubainishaji na Ufuatiliaji wa Mifugo na ustawi wa wanyama. Zaidi ya hayo, upelekaji wa mifugo kati ya masoko madogo na makubwa unaongeza utegemezi wa usafirishaji kwa njia ya reli au barabara ukichangia thamani kubwa ya ardhi kwa ajili ya nyama au mifugo kama ukilinganisha na ilivyo Mashariki ya Kati, hivyo kuifanya kuwa na ushindani mdogo.[2]

Sekta ya ufugaji inachangia asilimia 30 ya Pato Ghafi la Kilimo. Katika mwaka 2012-2013 uzalishaji wa maziwa ulifikia lita bilioni 2.0 na nyama tani 563,086 (nyama ya ng'ombe 309,353, kondoo na mbuzi 120,199 na nguruwe 79,274). Biashara ya mifugo ilishuhudia ngombe 1,215,541, mbuzi 960,199 na kondoo 209,292 katika soko la ndani wenye thamani ya kiasi cha Sh. bilioni 989.3.2 Usafirishaji nje ya nchi ya nyama ulifikia nyama ya ng'ombe tani 2.8, mbuzi tani 1,048 na tani 58.97 za nyama ya kondoo, uliofikia thamani ya kiasi cha Sh.bilioni 36.17.[3]

2 Kwa mfano, thamani ya nyama iliyotoka nchini Tanzania kuingia katika Jamhuri ya Falme za Kiarabu ni Dola za Marekani 3.8 kwa kilo moja, ikilinganishwa na Dola za Marekani 2.4 kwa nyama iliyotoka Australia.

3 Dola ya Marekani 1 = inakadiriwa kuwa Tsh. 1,500

Sehemu kubwa ya mifugo hiyo inatoka katika maeneo ya wafugaji asili. Nyanda za malisho ni rasilimali muhimu katika uzalishaji wa mifugo hii. Ulishaji wa mifugo katika misimu ya mvua na ukame, na maji, na uhamaji baina yao ni sehemu muhimu za nyanda za malisho. Mara nyingi sehemu za malisho na wakati mwingine maji hutumiwa kwa kushirikiana baina ya vijiji na kunaweza kuwa na ugumu wa kuyapata na taratibu za usimamizi. Kuelewa mgawanyo wa rasilimali hizi, hali yake na changamoto zozote au matatizo katika kuzipata ni muhimu katika kupanga mipango ya matumizi bora ya ardhi ya kijiji katika maeneo ya wafugaji. Zana nzuri kwa uchanganuzi kama huu ni uchoraji shirikishi wa ramani ya rasilimali za nyanda za malisho, ambayo inatoa fursa kwa jamii kuelezea matumizi yao ya rasilimali na kuanza kufafanua namna rasilimali hizi zinavyoweza kulindwa na kutumiwa kwa ushirikiano. Mchakato shirikishi wenyewe unaziwezesha jamii na kutoa fursa kwa makundi tofauti ndani ya jamii kuchangia katika mchakato mzima.

Wizara ya Maendeleo ya Mifugo na Uvuvi imetekeleza jukumu kubwa katika mchakato wa uandaaji wa Mwongozo huu wa Uwandani baada ya kuchukua nafasi ya kwanza kutathimini zana hii na kisha matumizi yake kupitia Mradi wa Usimamizi Endelevu wa Nyanda za Malisho. Wizara inazihimiza sekta zote zinazotaka kuelewa vizuri mgawanyo wa rasilimali za ufugaji na matumizi yake, kutumia mbinu hii.

*Dr Maria Mashingo,*
Katibu Mkuu Mifugo
Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi



# Yaliyomo

Kwa nini Uchoraji shirikishi wa ramani ya rasilimali nyanda za malisho unahitajika katika kuandaa mpango wa matumizi ya ardhi ya kijiji? 14
Kuelewa na kuandaa usimamizi endelevu wa ardhi ya malisho 15
Ushiriki na Ujumuishaji wa Mipango ya matumizi bora ya ardhi 16
Kulinda ushirikianaji wa rasilimali 20
Kuokoa muda na gharama 21
Kubadili mkabala, mtazamo na tabia 22
Jinsi ya kutumia mwongozo huu 23

**Ngazi ya 1** Matayarisho: kuandaa uchoraji wa ramani 25

*Hatua ya 1* Weka malengo ya uchoraji ramani 28
Uelewe mchakato mzima 29
Tembelea eneo linalochorwa ramani na jamii itakayokuwa inachora ramani 29
Bainisha malengo ya uchoraji ramani 29
Andaa orodha hakiki ya maswali kwa taarifa za ziada zinazotakiwa 31

*Hatua ya 2* Unda timu ya uwezeshaji 32
Mwezeshaji wa uchoraji ramani 33
Mchukua taarifa 34
Anayenakili ramani 34

*Hatua ya 3* Kubainisha washiriki wa uchoraji wa ramani na mipangilio mingine 38
Kubalianeni nani atashiriki katika zoezi la uchoraji ramani 39
Kubalianeni wapi na lini zoezi la uchoraji ramani litafanyika 42
Fanya mkutano wa utambulisho 43
Andaa vifaa vya uchoraji wa ramani 45
Chapisha orodha ya uchoraji wa ramni ya rasilimali ya ardhi ya malisho 45

## **Ngazi ya 2** Uwezeshaji: Kuchora ramani 47

*Hatua ya 4* Chora ramani ya nyanda za malisho 50
Wezesha ufunguzi wa zoezi hili na utambulisho 51
Anza kuchora ramani 52
Weka ufunguo wa ramani pamoja na alama na rangi zinazofaa 54
Andika majadiliano yote yanayoandamana na zoezi hilo 54
Amua muda unaofaa kwa mapumziko na kufunga 55

*Hatua ya 5* Ongeza Taarifa 58
Majadiliano yatakayozingatiwa na kikundi cha uchoraji ramani ili kuongeza taarifa 59
Kuchora ramani ya uhamaji na njia za mifugo 59
Kuchora ramani ya rasilimali muhimu na/au rasilimali zinazohitaji usimamizi maalumu 63
Kuongeza mipaka na migawanyo ya matumizi ya ardhi 64

*Hatua ya 6* Kamilisha ramani 66
Mwezeshaji 67
Mchukua Taarifa 67
Anayenakili ramani 67

## **Ngazi ya 3** Uthibitisho: Kuhakikisha ramani 71

*Hatua ya 7* Washirikishe wadau 74
Andaa mkutano wa kupata maoni 75
*Hatua ya 8* Andika ripoti 78
*Hatua ya 9* Rudisha ramani kwa jamii na washirikishe na wadau wengine 81

## **Ngazi ya 4** Matumizi: Kutumia ramani 85

*Hatua ya 10* Mipango 88
*Hatua ya 11* Usimamizi 94
*Hatua ya 12* Ufuatiliaji na tathmini 96

## Kiambatisho

Orodha ya Uchoraji wa ramani ya rasilimali za nyanda za malisho 99

# Kwa nini Uchoraji shirikishi wa ramani ya rasilimali nyanda za malisho unahitajika katika kuandaa mpango wa matumizi ya ardhi ya kijiji?



Uchoraji shirikishi wa ramani ya rasilimali za nyanda za malisho ni mchakato wa thamani na seti ya shughuli kwa ajili ya uelewa mzuri na kujenga usimamizi endelevu wa nyanda za malisho katika kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi ya kijiji na michakato mingine ya mipango na usimamizi. Unatoa nafasi kwa jamii kuchangia kwa dhati katika michakato ya mipango na ufanyaji maamuzi kama sehemu ya mkabala jumuishi wa mipango shirikishi ya matumizi bora ya ardhi, kama ilivyoelezwa katika sera ya taifa, sheria na miongozo. Uchoraji shirikishi wa ramani ya rasilimali za nyanda zamalisho pia unaweza kuokoa muda na gharama.

## Kuelewa na kuandaa usimamizi endelevu wa ardhi ya malisho

Uchoraji wa ramani ya rasilimali za nyanda za malisho ni nyenzo yenye nguvu ya kutoa taarifa. Zoezi la kuchora ramani ni sehemu nzuri ya kuanzia katika majadiliano ya ngazi ya jamii kuhusu rasilimali na masuala ambayo yanaizunguka jamii husika. Ramani shirikishi za rasilimali za nyanda za malisho zinaweza kutumika kubainisha na kuelewa matumizi ya ardhi ya malisho ya wafugaji, maeneo tofauti zilipo rasilimali, upatikanaji wa rasilimali na misimu ya upatikanaji wa rasilimali. Ramani shirikishi za rasilimali za nyanda za malisho zinaonyesha taarifa muhimu kama vile huduma za matibabu ya mifugo, miundombinu ya masoko, mipaka ya matumizi ya ardhi na uhamaji wa mifugo. Majadiliano yenye lengo ambayo yanafanyika wakati na baada ya zoezi la uchoraji ramani yanaweza kubainisha matatizo na changamoto za usimamizi wa nyanda za malisho na kusababisha uchanganuzi wa uchaguzi wa suluhisho kwa usimamizi mzuri na endelevu wa rasilimali za nyanda za malisho.

Ramani shirikishi inatoa rekodi ya kielelezo cha eneo na rasilimali zake. Uchoraji wa ardhini (kwenye ardhi) au uchoraji wa mchoro (kwenye karatasi) unawakilisha alama muhimu za ardhi zilizobainishwa na jamii kutoka angani. Ramani

hizi hazitegemei vipimo halisi, bali zinaonyesha ukubwa unaokaribiana na nafasi za sifa zinazokaribiana. Uchoraji shirikishi wa ramani ni sehemu nzuri ya kuanzia kwa ajili ya kujadili rasilimali muhimu na masuala yanayohusiana na ardhi. Pia inasaidia kutambulisha na kugundua pamoja na jamii dhana za uchoraji ramani, ukiwawezesha kuonyesha ugawaji wa rasilimali na kubainisha sehemu muhimu. Picha inaandika maneno elfu moja.

Ramani shirikishi ya rasilimali za nyanda za malisho inaweza pia kutumika kwa ajili ya kupatana na kutayarisha shughuli za usimamizi wa nyanda za malisho – kueleza matatizo na changamoto ambazo utatuzi wa usimamizi wa rasilimali unahitaji kupatikana na kufanywa kuwa sheria. Ramani za rasilimali za nyanda za malisho zinatoa data muhimu za msingi kwa ajili ya ufuatiliaji na tathmini iliyopo ndani ya mifumo ya usimamizi wa nyanda za malisho inayobadilika. Ramani ya rasilimali, na taarifa zake zote zinazoambatana nayo, zinatumika kama kigezo cha kufuatilia mabadiliko kwa kipindi fulani.

## Ushiriki na Ujumuishaji wa Mipango ya matumizi bora ya ardhi

Nchini Tanzania, uandaaji shirikishi wa mpango ya matumizi bora ya ardhi ya kijiji unaongozwa na Sheria ya Ardhi ya Vijiji Na. 5 (1999) na kanuni zake za mwaka 2002 na pia kwa Sheria ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi Na. 6 (2007). Sheria ya Ardhi ya Vijiji (Kifungu cha 12 na 13) inatoa madaraka kwa Halmashauri za Vijiji na taasisi zake kuandaa mipango shirikishi ya matumizi bora ya ardhi ya kijiji. Sheria ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (chini ya Kifungu cha 18, 22 na 35) inaeleza uundaji wa mamlaka za mipango, kazi na taratibu za kuandaa mipango shirikishi ya matumizi bora ya ardhi ya kijiji na michakato ya uidhinishaji.

Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi imebainisha wafugaji na wawindaji-wakusanya matunda na mizizi kama makundi yaliyo katika mazingira magumu yanayohitaji uangalizi. Mazingira hayo magumu yanaletwa na

ukosefu wa usalama wa ardhi ambao wafugaji na wakusanya matunda walikuwa nao, na katika mazingira mengine bado wanao usalama huo.

Miongozo ya Tume ya Taifa ya Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi ya Uandaaji wa Mipango ya Matumizi ya Ardhi ya Kijiji, Utawala na Usimamizi nchini Tanzania ya mwaka 2011 (toleo lililopitiwa upya) inaeleza hatua kuu sita za kufuata wakati wa kuandaa mipango shirikishi ya matumizi ya ardhi ya kijiji:

- Maandalizi ngazi ya wilaya;
- Tathmini shirikishi vijijini;
- Uchoraji ramani ya matumizi ya ardhi ya kijiji yaliyopo;
- Kupanga Mipango shirikishi ya matumizi bora ya ardhi ya kijiji;
- Utekelezaji wa utawala wa ardhi ya kijiji:
- uongezaji wa usalama wa umiliki;
- Usimamizi wa matumizi ya ardhi ya kijiji.



Ujumuishaji wa kupanga mipango shirikishi ya matumizi bora ya ardhi ni mchakato wa wazi na wa uwajibikaji ambapo jamii husika inachukua jukumu la kati la kufanya maamuzi yanaohusiana na ardhi na rasilimali ambazo wanazitumia. Mkabala unalenga kubainisha matumizi bora ya ardhi na rasilimali kupitia mazungumzo baina ya maslahi tofauti kwa kuzingatia usawa, ufanisi, kujitosheleza, uhifadhi na uendelevu. Mipango shirikishi ya matumizi ya ardhi inatoa muundo na jukwaa kwa wadau kukutana, kuwasiliana, kuunda mikakati na kuitekeleza kwa pamoja.

Uchoraji shirikishi wa ramani ya rasilimali za nyanda za malisho ni nyenzo muhimu katika uandaaji wa mipango hiyo. Ramani shirikishi zinaziruhusu jamii kujieleza wazi kupitia uelewa wao wenyewe wa mandhari na rasilimali zake asili. Ramani hizo zinaweza kutoa mbadala kwa lugha, picha, na maneno yaliyoandikwa ya wale ambao wanaweza kuwa na madaraka zaidi katika jamii. Ramani hizi zinaweza kuzipa madaraka jamii husika kwa sababu zinawapa njia ya kujiwakilisha zenyewe. Kwa sababu wanajamii wanatengeneza ramani wao wenyewe, wanahisi kuwa wamiliki zaidi na kuendelea kuwa na mapenzi katika matumizi yao.



Mjadala unaohusishwa na  uandaaji wa ramani shirikishi unawapa wanaume, wanawake, watoto na watu tofauti toka makundi tofauti ya vipato na ustawi  fursa ya kushirikiana kuandaa picha ya kielelezo kinachoonekana cha  mandhari, malisili na makazi na mifumo ya matumizi ya ardhi. Ukifanyika vizuri, uchoraji ramani unaweza kuongeza uelewa wa jamii ya makundi tofauti ya watumiaji na kujituma katika kusimamia vizuri rasilimali zao asili. Kwa kufanya kazi na wawakilishi wa jamii katika kutengeneza ramani ya rasilimali za nyanda za malisho pia kunaweza kujenga uelewa na kujiamini kwa wafanyakazi wa maendeleo na wa ugani. Kutumia mikabala shirikishi kunabadilisha matokeo kuwa mazuri zaidi kwa kujenga upya maeneo yaliyokuwa yameharibika.

Mchakato wa kuhifadhi nyaraka za matumizi ya rasilimali (kwa vielelezo na maneno) kama sehemu ya tathmini shirikishi ya vijijini, sio tu unaziwezesha jamii bali pia unaweka msingi wa kujumuisha na kusaidia mambo kama kuhama kwa mifugo na makubaliano kati ya vijiji kuhusiana na kushirikiana rasilimali. Pia unatoa fursa ya kuzingatia aina zote tofauti za matumizi ya ardhi ikiwemo kilimo, uchimbaji madini na makazi, na namna ya kusuluhisha migogoro ambayo inaweza kuwepo kati ya hayo na uzalishaji wa mifugo. Taarifa hizi zinaunda msingi wa Hatua ya 4, 5, na 6 katika mchakato wa  kuandaa mipango ya matumizi bora ya ardhi ya vijiji (kama hapo juu ), ambapo ramani shirikishi za rasilimali na ripoti zinazoambatana nazo zinaweza kutumiwa kama nyaraka za uthibitisho.



### Kulinda ushirikianaji wa rasilimali

Sheria ya Ardhi ya Vijiji (1999) ina vifungu ambavyo vinaonyesha utambuzi wa mali ya pamoja kwa wafugaji, kiasi kwamba utaratibu wa kushirikiana ardhi hiyo unawezekana, ikiwemo utoaji wa Vyeti vya haki Miliki ya Kimila kwa ardhi iliyo chini ya umiliki wa ufugaji (kifungu cha 29.2 (iii)). Hata hivyo, tatizo linabakia kwenye kufafanua umiliki wa sasa wa ufugaji na utumiaji – ni namna gani wafugaji wanapata, kushikilia na kuachia ardhi.

Zaidi ya hayo, Sheria ya Rasilimali za Ardhi ya Kuchungia na Chakula cha Wanyama (Na. 10, 2010, Kifungu 17(3)) kinaonyesha kutoa ulinzi fulani kwa wafugaji:

> "Kulingana na sheria zilizopo, Halmashauri ya Kijiji itapiga marufuku, kuzuia, kukataza au kudhibiti uingiaji katika eneo la malisho kwa madhumuni ya kulima, kuchimba madini, uanzishaji wa eneo tengefu la wanyamapori au matumizi mengine yoyoye tofauti na ufugaji wa mifugo."

Aidha, Sheria inaeleza kwamba Halmashauri ya Kijiji itenge sehemu ya ardhi ya jumuiya kama eneo mkakati la kuchungia kulingana na Sheria ya Mipango ya Matumizi ya Ardhi (2007).

Pale ambapo vijiji vinashirikiana rasilimali, Sheria (mahususi zaidi Sheria ya Ardhi ya Vijiji Kifungu cha 11 na Kifungu cha 58; na Sheria ya Mipango ya Matumizi Bora ya Ardhi, Kifungu cha 18 na Kifungu cha 33) zinasisitiza kwamba vijiji viandae mpango wa sekta ya usimamizi wa rasilimali za kijiji pamoja na mpango wao wa matumizi bora ya ardhi ya kijiji ili kutoa ushirikianaji wa rasilimali kati ya idadi ya vijiji na kwa uhamaji wa mifugo wa kuvuka katika mipaka ya vijiji. Mpango wa sekta ya usimamizi wa rasilimali unapaswa kushughulikia na kuwezesha kushirikiana rasilimali, na unapaswa kujumuishwa katika mipango ya muundo wa matumizi ya ardhi ya wilaya.

Makubaliano na usimamizi wa mipango ya kisekta na sheria ndogo vinaweza kutoa muundo rasmi wa17 kushirikiana rasilimali yenye maelekezo yanayowezesha majirani kutumia rasilimali zilizopo, namna gani na lini wanaweza kuzitumia. Hili inaweza kuhalalisha zaidi namna ya kushirikiana rasilimali za nyanda za malisho kama vile maeneo la kuchungia mifugo.

Ili kuandaa michakato hii tofauti yenye utofauti kimiundo na kimipango, taarifa inatakiwa kuhusu rasilimali za nyanda za malisho na upatikanaji unaohusiana na taratibu za usimamizi. Uchoraji wa ramani ya rasilimali za nyanda za malisho ni mchakato muhimu na zana ya kuwezesha kushirikiana rasilimali. Kwa mfano, pale ambapo vijiji vitatu vinashirikiana rasilimali, uchoraji wa ramani ya rasilimali ya nyanda za a malisho unaweza kufanywa na vijiji vitatu kwa wakati mmoja (kama vinapakana) ili kuonyesha ni wapi na namna gani wanashirikiana rasilimali.

### Kuokoa muda na gharama

Ugumu wa kushughulikia masuala changamani ya matumizi mengi na uhamaji katika maeneo ya ufugaji mara nyingi unawakatisha tamaa watengenezaji na wasimamizi wa mipango ya ardhi, na ukosefu wa muda wa udhibiti wa rasilimali na watumishi wa kuelewa kikamilifu hali halisi na/au mazungumzo marefu au utatuzi wa migogoro. Hii ina maana kwamba michakato na matokeo mara nyingi huleta upinzani, ikisababisha matatizo kurudia kujitokeza tena baadaye.

Kupanga mpango ya matumizxi bora ya ardhi ya kijiji unaweza kuwa mchakato wa gharama, hususan pale ambapo kuna ukosefu wa taarifa zilizo tayari kuhusu matumizi ya rsilimali, au pale ambapo kuna migogoro kuhusu mipaka na/au baina ya pande tofauti.. Uchoraji shirikishi wa ramani ya nyanda za malisho unaweza kusaidia kupunguza gharama za uandaaji wa mipango ya matumizi bora ya ardhi ya vijiji kwa sababu ni njia inayofaa ya kukusanya taarifa za kina kuhusu matumizi ya rasilimali ya wenyeji na kuanzisha majadiliano ya kushirikiana rasilimali na/au migogoro inayohusiana. Uchoraji ramani shirikishi huwa una gharama ndogo na hautegemei teknolojia ngumu.

Ramani ya rasilimali ya nyanda za malisho inaweza kuandaliwa katika muundo wa kipindi cha muda mfupi na kisha inaweza kuchapishwa, kutolewa tena , kuongezewa na kuhuishwa.

Taarifa zinaweza kutumiwa katika namna mbalimbali kwenye mipango na ufuatiliaji, ikiwa ni pamoja na kuhamishia katika mifumo ya taarifa za mfumo wa kijiografia au ramani za 'Google Earth' (tazama Hatua ya 4 ya miongozo hii).

Wakati huohuo, uchoraji ramani unasisitiza maeneo yenye matatizo ambayo yanaweza kushughulikiwa na kutatuliwa na jamiii yenyewe ili kufikia muafaka. Kama taarifa zote zinazohitajika zitakusanywa na kuwezesha kutatuliwa kwa kile ambacho kilikuwa kutoelewana kokote ndani ya jami, kabla ya mchakato "rasmi" wa kupanga mpango wa matumizi ya ardhi kufanyika, hili litaokoa muda na gharama zinazohusiana na viongozi wa serikali, kwa kuwa watahitaji kutumia muda mchache kuwa na jamii wakiandaa mipango ya matumizi ya ardhi ya kijiji.

## Kubadili mkabala, mtazamo na tabia

Kama unataka "ushirikishwaji" uwe wa manufaa, kiwango cha juu cha ushirikishwaiji inabidi kidhamiriwe. Hapa ndipo wafugaji, wanafanya kazi kwa ushirikiano na kusaidiwa na wakala wa maendeleo, wanafanya maamuzi yote kuhusiana na usimamizi ndani ya maeneo ya usimamizi wa nyanda za malisho, kama ilivyoelezwa katika mpango wa matumizi ya ardhi ya kijiji na makubaliano mengine yanayohusiana.

Kufikia kiwango hiki cha juu cha ushirikishwaji kutahusisha kubadili mitazamo na kubadili tabia kwa wasomi wengi – yaani, mabadiliko ya wanachokifikiria na namna wanavyofanya kazi. Kiini cha mabadiliko haya ni kwa wasomi kuwa wawezeshaji zaidi kuliko kuongoza au kudhibiti, na wataalamu, waanzishe uhusiano wa kusaidia na kujenga uwezo na kufanya ushirikishaji ambao unawezesha jamii za wenyeji kurejesha udhibiti mkubwa wa kutawala na kuendesha maisha yao.

## Jinsi ya kutumia mwongozo huu

Mwongozo huu wa uchoraji shirikishi wa ramani ya rasilimali za nyanda za malisho umeundwa kwa kuweza kutumika kirahisi katika kazi za ugani katika jamii. Katika kila sehemu, mchakato wa uchoraji wa ramani ya rasilimali za nyanda za malisho umegawanywa katika hatua tofauti, na kisha katika kila hatua wataalamu wanapewa mwongozo wa wazi wa hatua kwa hatua wa jinsi ya kufanya kila shughuli maalumu.

Miongozo inaeleza madhumuni, mbinu na matokeo yanayotarajiwa kwa kila hatua kuu za uchoraji ramani na hatua mbalimbali katika kila hatua kuu. Visanduku kinatoa mifano na mpangilio kwa wataalamu kuzingatia.

Inapendekezwa kwamba wataalamu wapitie mwongozo na jamii wanayofanya nayo kazi, wapitie kila ngazi na hatua muhimu moja baada ya nyingine katika mpangilio uliowekwa. Hata hivyo, sehemu za mchakato wa uchoraji ramani zinaweza kuhitaji kufuatwa katika muktadha wa wenyeji, ili kuakisi madhumuni na malengo ya kazi maalumu ya uchoraji ramani au kushughulikia mahitaji na vipaumbele vya jamii tofauti katika eneo husika.



# Ngazi ya 1

## Matayarisho: kuandaa uchoraji wa ramani

Ngazi ya 1 inalenga katika kuandaa uchoraji wa ramani. Hatua za hapa ni:

- Hatua ya 1. Weka malengo ya kuchora ramani
- Hatua ya 2. Unda timu ya uwezeshaji
- Hatua ya 3. Bainisha washiriki wa uchoraji wa ramani







# Hatua ya 1

## Weka malengo ya uchoraji ramani

*Kabla ya kuendelea mbele na zoezi la uchoraji wa ramani, kuna baadhi ya hatua muhimu za matayarisho na shughuli za kukamilisha. Katika hatua hii ya kwanza, mtaalamu anafafanua hasa kwa nini uchoraji wa ramani ya rasilimali za nyanda za malisho inabidi ufanyike. Wanajaribu kuonyesha nini kwenye ramani? Kuweka malengo ya uchoraji ramani kutalenga katika shughuli na kuhakikisha kwamba matokeo ya ramani shirikishi ya rasilimali za nyanda za malisho yanajumuisha taarifa zinazotakiwa. Malengo ya wazi yatamsaidia mtaalamu kuelezea zoezi la uchoraji ramani kwa jamii. Kukamilisha hatua zifuatazo kutasaidia kuandaa malengo ya wazi na mazuri.*

### Uelewe mchakato mzima

Kuwa na ufahamu wa, kujisikia vizuri na, na kujiamini katika mchakato mzima wa uchoraji ramani ni muhimu kwa kuhakikisha msingi mzuri kwa ajili ya mchakato mzima – hii baadaye itasaidia kuendeleza uelewa wa pamoja wa mchakato na utekelezaji wake mzuri. Soma mwongozo mzima angalau mara mbili kabla ya kufanya zoezi la uchoraji ramani.

### Tembelea eneo linalochorwa ramani na jamii itakayokuwa inachora ramani

Inapendekezwa kulitemnbelea eneo litakalochorwa ramani. Tembelea eneo na jamii na ifahamu jiografia ya eneo husika na maliasili iliyopo. Ziara hiyo inaweza pia kutumika kuanza kujihusisha na jamii ya wenyeji na kujenga kuaminiwa na kuanzisha uhusiano nao. Watembelee pia wawakilishi wa serikali za mtaa ili kuwaarifu kuhusu kazi ya uchoraji ramani iliyopangwa na kuwaalika kufuatilia mchakato mzima

### Bainisha malengo ya uchoraji ramani

Malengo ya kuchora ramani yanapaswa kuakisi lengo la msingi na mahitaji ya shughuli; mfano, Mpango wa matumizi bora ya ardhi ya kijiji ulioandaliwa vizuri (wa pamoja/binafsi) ambao utatoa matumizi endelevu na kushirikiana rasilimali. Malengo yawe wazi na mahususi. Kuwa mwangalifu usitake kukamilisha mambo mengi kupita kiasi katika zoezi moja la uchoraji ramani – ni vizuri kuanza na lengo moja la wazi na rahisi kuliko kujaribu kukamilisha mambo kadhaa ambayo ni magumu. Kama ni lazima, zoezi la kuchora ramani linaweza kufuatiwa na mahojiano zaidi ya kina au majadiliano ya kikundi lengwa kidogo.

Mifano ya malengo ya uchoraji ramani ya rasilimali nyanda za malisho inajumuisha:

- » Kubainisha na kutoa uelewa wa maliasili katika eneo la usimamizi wa nyanda za malisho – hii inaweza kujumuisha kijiji kimoja au inaweza kujumuisha vijiji vingi kama vinashirikiana rasilimali kama vile eneo la kuchungia mifugo au maji.
- » Kubainisha na kuelewa matatizo na masuala yanayohusiana na rasilimali za nyanda za malisho.
- » Kutoa ramani shirikishi ya rasilimali za nyanda za malisho ya eneo la malisho linalosimamiwa, ambayo itatumiwa kama msingi wa mazungumzo na utekelezaji wa mpango wa matumizi bora ya ardhi ya kijiji utakaofanywa na wadau mbalimbali, na pia kama sehemu muhimu ya nyaraka za makubaliano na mpango wa usimamizi wa nyanda za malisho.
- » Kutoa chanzo cha taarifa ambayo inatumika katika michakato ya Ufuatiliaji na Tathmini kwa ajili ya usimamizi uliorekebishwa.

Malengo mahususi zaidi ya uchoraji ramani yanaweza kuwa:

- » Kubainisha na kupanga katika makundi maliasili muhimu katika eneo.
- » Kuelewa rasilimali muhimu (au za kipaumbele) na jukumu lake katika eneo la nyanda za malisho.
- » Kuelewa mwelekeo wa uhamaji (mifugo na watu) ndani na nje ya eneo.
- » Kuelewa hali halisi ya rasilimali, na maeneo ya nyanda za malisho yanayoweza kuhitaji ulinzi au usimamizi maalumu.
- » Kuelewa matumizi tofauti ya ardhi katika eneo la usimamizi wa nyanda za malisho, na maeneo ambayo matumizi ya ardhi yako katika mgogoro.



## Andaa orodha hakiki ya maswali kwa taarifa za ziada zinazotakiwa

Taarifa za ziada zitatakiwa ili kuongezea katika ramani shirikishi za rasilimali za nyanda za malisho ili kukamilisha malengo ya kuchora ramani. Kwa mfano, kama unajaribu kubainisha au kuonyesha maeneo ya mabadiliko ya matumizi ya ardhi au masuala mengine muhimu yanayohusiana na ardhi, inaweza kuwa muhimu kuuliza maswali kuhusu ardhi inapatikanaje na na namna inavyodhibitiwa. Taarifa zinaweza kukusanywa ama wakati wa hatua ya kuchora ramani au wakati wa majadiliano ya vikundi lengwa, ambavyo vinaweza kufanyika kwa pamoja na zoezi la kuchora ramani hapo baadaye. Orodha ya maswali ya kuongoza majadiliano inapaswa kuandaliwa kabla ya zoezi la uchoraji.



# Hatua ya 2

## Unda timu ya uwezeshaji

*Mafanikio ya mchakato wa kuchora ramani yatategemea ujuzi wa timu ya uwezeshaji. Kuna majukumu makuu matatu ya kukamilisha – yale ya mwezeshaji wa kuchora ramani, mwandika taarifa, na mchora ramani (ingawa jukumu la mchukua taarifa na anayenakili ramani yanaweza kuunganishwa kama kuna uhaba wa wafanyakazi). Angalau mmoja wa wanatimu (vizuri zaidi mwezeshaji wa uchoraji) awe amefanya zoezi la uchoraji ramani kabla.*

Timu halisi ya uwezeshaji ihakikishe kwamba:

- Ina angalau mjumbe mmoja anayejulikana kwa jamii na ana kiwango kikubwa cha uhusiano na jamii na wanamwamini.
- Wajumbe wote wawe wanazungumza lugha ya wenyeji.
- Wajumbe wote wawe wanaelewa utamaduni wa wenyeji, desturi na maadili ya kijamii, kisiasa, na muktadha wa mazingira na historia.

Angalau mjumbe mmoja awe mwanamke, kwa kuwa mtazamo na uelewa wa mazingira ya mwanamke unaweza kuwa tofauti na ule wa wanaume.

Inaweza kusaidia kuwa na mjumbe wa timu ya Usimamizi Shirikishi wa Matumizi Bora ya Ardhi wa wilaya wakati wa zoezi la kuchora ramani, ili waweze kuelewa vizuri mchakato ambao umefuatwa na wanajamii na majadiliano yaliyoambatana nao.

### Mwezeshaji wa uchoraji ramani

Jukumu kuu la mwezeshaji wa uchoraji wa ramani ni kuhamasisha na kuliwezesha kundi la jamii kutengeneza au kuchora ramani ya rasilimali ya nyanda za malisho. Mwezeshaji atatakiwa kutoa maelezo ya wazi ya malengo ya mchakato wa kuchora ramani na kuisaidia jamii kubainisha aina ya taarifa wanayotaka kuwasilisha kwenye ramani. Aidha, mwezeshaji atatakiwa kuandaa taarifa ambayo kimsingi ilibainishwa kupitia kutoa mapendekezo, uulizaji mzuri wa maswali, na kwa kuhamasishwa. Ili kufanya hivyo, mwezeshaji atahitaji ujuzi maalumu (tazama kisanduku cha 1).

## Mchukua taarifa

Mchukua taarifa anahusika na kuandika taarifa za kina za majadiliano ya kikundi na majibu ya maswali kutoka kwa mwezeshaji. Kuandika taarifa kwa usahihi ni muhimu sana, kwa kuwa taarifa hizo zitakuwa msingi wa mipango ya usimamizi inayofuatia. Mwandishi atahitaji ujuzi maalumu katika kusikiliza, kuangalia na kurekodi, na ataweza kufuatilia majadiliano kadhaa kwa mara moja na kuchukua pointi muhimu.

## Anayenakili ramani

Wakati wa uchoraji wa ramani ya rasilimali ya nyanda za malisho unaofanywa na jamii, jukumu la anayenakili ramani litakuwa ni kuhakikisha kwamba alama zote zimeonyeshwa kwa uwazi au kupewa majina, na zinaeleweka. Mchakato unaweza kusimamishwa kama kuna upungufu unaohitaji kujazwa. Mchoraji atahitaji kunakili kwa uangalifu taarifa zote ambazo jamii imezionyesha katika ramani yao. Ramani iliyochorwa itatakiwa kuwa wazi kadri iwezekanavyo, ikiwa na ufunguo unaoelezea vipengele mbalimbali vya taarifa na alama zilizotumika. Hii inaweza kuwa katika kipimo kidogo kuliko ramani iliyochorwa na jamii, lakini lazima iwe na usahihi.

### Kisanduku cha 1: Ujuzi wa timu nzuri ya uwezeshaji

*Mwezeshaji mzuri ni yule ambaye…*

- Anawahamasisha washiriki kuwa na hisia za motisha, kuthaminiwa na kuwa tayari kushiriki;
- Anakamilisha uchoraji kupitia zoezi ambalo washiriki wanahisi wanalimiliki pamoja na kulidhibiti yaani, mchakato haudhibitiwi na mwezeshaji peke yake;
- Anawafanya washiriki wazingatie shughuli waliyonayo na mada ambayo imechaguliwa, wakati huohuo hakosi fursa za kugundua mada zisizotarajiwa lakini muhimu;
- Anaonyesha kujali hisia/mahitaji ya washiriki na kufuata somo ili kuendana na mahitaji yao, wakati huohuo akilinda mchango wa kila mmoja usidharauliwe;
- Anasimamia kutowiana kwa madaraka ndani ya kikundi, akihakikisha kwamba kila mtu ana fursa ya kushiriki na kwamba hakuna mtu anayehisi kama tengwa au kulazimishwa kushiriki;
- Anahakikisha kwamba zoezi la uchoraji linaanza katika muda uliokubaliwa, na kukamilika ndani ya muda uliokubaliwa, bila ya washiriki kuhisi kuharakishwa. Kama kiwango cha ushiriki kinaanza kupungua au kutawaliwa na mjumbe mmoja au zaidi, zoezi linapaswa kusimamishwa na kupangwa upya.
- Hamasisha mazungumzo na majadiliano baina ya washiriki na makundi yanayopenda, lakini sikiliza zaidi kuliko kuzungumza;

» Elewa ni muda gani mwafaka kuingilia kati katika zoezi ili kutatua mabishano, au kujaza mapungufu yaliyojitokeza, bila ya kuharibu mtiririko wa zoezi au majadiliano;

» Changamsha kikundi au kitulize kama itahitajika.

*Mchukua taarifa mzuri ni yule ambaye…*

» Anasikiliza kwa umakini, ikiwa ni pamoja na kusikiliza mazungumzo yote wakati watu kadhaa wanazungumza kwa wakati mmoja;

» Anaandika pointi zilizotolewa kwa usahihi, ikiwa ni pamoja na sehemu kuu ya majadiliano na maoni yoyote maalumu yanayovutia;

» Anawianisha haja ya kurekodi pamoja na maelezo kadri iwezekanavyo kuendana na kasi ya majadiliano na utoaji wa taarifa;

» Anafuatilia ushiriki maalumu wa vikundi mbalimbali (wanaume na wanawake, na vikundi vyenye maslahi tofauti) na kumsaidia mwezeshaji kuhakikisha anahusisha watu wote na kuepuka upendeleo;

» Anathamini lugha ya ishara za mwili, utoaji ujumbe "bila kuzungumza", na anaonyesha panapojitokeza wasiwasi na mvutano;


» Anamsaidia mwezeshaji kubainisha  mapungufu yaa taarifa na kutatua kutoelewana kokote;

» Anashughulikia mambo kikamilifu, ikiwa ni pamoja na maelezo ya mahali, muda wa kuanza na kumaliza, na majina ya washiriki wote.

*Anayenakili ramani mzuri (mchoraji) ni yule ambaye…*

- Anaelewa kikamilifu na kutafsiri kile wanajamii wanachojaribu kusema kupitia mchoro wao ili kumsaidia mwandishi;
- Kufuatilia kinachochorwa na kwa mpangilio upi, ili kuweza kubainisha vipengele ambavyo vimepewa umuhimu mkubwa na vyovyote ambavyo vinaweza kuwa vimesahaulika;
- Ana ujuzi wa kuchora ili kuwakilisha ramani kwa usahihi na kuiweka kwa vipimo kwenye karatasi ndogo;
- Anaweza kufanya kazi na wataalamu wa Mfumo wa Taarifa za Kijigrafia('GIS'), kama itaonekana inafaa, kuhamishia taarifa kwenye ramani ya dijitali.





# Hatua ya 3

## Kubainisha washiriki wa uchoraji wa ramani na mipangilio mingine

*Mara tu inapoanzishwa, timu ya uwezeshaji inatakiwa kukubaliana na viongozi wa jamii kuhusu nani atashiriki katika zoezi la uchoraji wa ramani, lini na wapi zoezi hilo litafanyika. Wajumbe wa Kamati ya Usimamizi wa Matumizi Bora ya Ardhi ya Kijiji wanapaswa kujumuishwa kwenye kundi la uchoraji ramani.*

*Kisha timu ya wawezeshaji itafanya mkutano wa ufunguzi na washiriki wa uchoraji wa ramani ili kuhakikisha kwamba wanaelewa mchakato huu na sababu muhimu za uchoraji ramani, tatua kutoelewana kokote, na panga lojistiki zote za hili zoezi.*

*Inaweza kuwa muhimu kuwajulisha au kupata makubaliano ya viongozi wa serikali za mitaa kama vile Timu ya Maumizi Bora ya Ardhi ya wilaya ili kuchora ramani.*

### Kubalianeni nani atashiriki katika zoezi la uchoraji ramani

Timu ya uchoraji ramani itajadiliana na jamii kuhusu nani atayewakilisha makundi ya wadau, ili kuwe na uwakilishi mzuri kutoka kwenye jamii, lakini lisiwe kundi kubwa sana kiasi cha kutolimudu (angalia Kisanduku cha 2). Kwa ajili ya michakato wa kupanga mpango wa matumizi bora ya ardhi ya kijiji inafaa kwa baadhi ya wajumbe wa Kamati ya Usimamizi wa Matumizi Bora ya Ardhi ya Kijiji kushiriki katika mkutano huu; hata hivyo, kundi la washiriki halipaswi kutokana na kundi hili tu. Badala yake, kundi litafakari migawanyiko ya kijamii katika umri, hadhi na uwezo. Upangaji kulingana na" uwezo" au "utajiri" unaweza kufanywa mapema ili kubainisha migawanyiko hii. Washiriki vijana wanaweza kutoa mchango mkubwa, kwa vile wanaweza kuona na kuwa na uzoefu tofauti wa nyanda za malisho tofauti na wakubwa wao.

Tunapozungumzia nyanda za malisho, ni muhimu kipekee kwamba wafugaji (wakiwemo wale wenye mtindo wa maisha ya kuhamahama) wajumuishwe.



Mnapaswa kujadiliana na wawakilishi wa jamii kama wanaume na wanawake wanaweza kufanya zoezi hilo kwa pamoja au kutahitajika shughuli za uchoraji wa ramani kufanywa tofauti. Kama wanaume na wanaawake wanakutana mara kwa mara na kujadili masuala yao kwa pamoja kwenye jamii, basi hakuna sababu ya kuwatenganisha. Kwa mtazamo wowote utakaotumiwa, ni muhimu kwamba wanaume na wanawake wawe na fursa sawa ya kuchangia.

### Kisanduku cha 2: Watu wangapi washiriki katika uchoraji wa ramani?

Madhumuni ya uchoraji shirikishi wa ramani ni kuipa jamii fursa ya kuchangia kwenye mchakato unaoathiri maamuzi yanayofanywa kuhusu ardhi, rasilimali na njia zao za kujipatia riziki. Kwa hiyo, ni muhimu ikiwa idadi kubwa ya washiriki wanaweza kushiriki katika uchoraji wa ramani. Hii pia inatoa fursa kwa sauti na matakwa tofauti kusikilizwa, na, iwapo jambo hili litafanyika vizuri, kutatoa jukwaa hai na tofauti kwa ajili ya kubadilishana taarifa. Kukiwa na timu ya wawezeshanji wenye uzoefu mzuri, makundi ya watu zaidi ya 20 yanaweza kushiriki.

Hata hivyo, kama kutakuwa na watu wengi katika kikundi cha uchoraji wa ramani, itakuwa vigumu kwa timu ya uwezeshaji kuratibu zoezi hili. Kama timu ya uwezeshaji haijiamini kumudu kundi kubwa basi watakubaliana na jamii kwamba idadi ndogo ya watu washiriki. Kiasi cha watu wapatao kumi wanaweza kuchaguliwa ili washiriki katika uchoraji ramani, wakati wengine wakiangalia na kushauri. Njia nyingine ni kuligawa kundi katika vikundi vidogovidogo vinavyofaa (wanaume/wanawake au watu wazima/vijana) na kutoa idadi kadhaa ya ramani

Madhumuni ya uchoraji shirikishi wa ramani ni kuipa jamii fursa ya kuchangia kwenye mchakato unaoathiri maamuzi yanayofanywa kuhusu ardhi, rasilimali na njia zao za kujipatia riziki. Kwa hiyo, ni muhimu ikiwa idadi kubwa ya washiriki wanaweza kushiriki katika uchoraji wa ramani. Hii pia inatoa fursa kwa sauti na matakwa tofauti kusikilizwa, na, iwapo jambo hili litafanyika vizuri, kutatoa jukwaa hai na tofauti kwa ajili ya kubadilishana taarifa. Kukiwa na timu ya wawezeshanji wenye uzoefu mzuri, makundi ya watu zaidi ya 20 yanaweza kushiriki.

Hata hivyo, kama kutakuwa na watu wengi katika kikundi cha uchoraji wa ramani, itakuwa vigumu kwa timu ya uwezeshaji kuratibu zoezi hili. Kama timu ya uwezeshaji haijiamini kumudu kundi kubwa basi watakubaliana na jamii kwamba idadi ndogo ya watu washiriki. Kiasi cha watu wapatao kumi wanaweza kuchaguliwa ili washiriki katika uchoraji ramani, wakati wengine wakiangalia na kushauri. Njia nyingine ni kuligawa kundi katika vikundi vidogovidogo vinavyofaa (wanaume/wanawake au watu wazima/vijana) na kutoa idadi kadhaa ya ramani

## Kubalianeni wapi na lini zoezi la uchoraji ramani litafanyika

Jadiliana na jamii lini na wapi zoezi la uchoraji wa ramani litafanyika. Hii iwe wakati unaofaa kwa jamii na uendane na majukumu yao ya kila siku/msimu na kazi (wote wanaume na wanawake). Itakuwa vigumu kwa jamii kutenga muda kwa ajili ya uchoraji wa ramani wakati kazi zao zikiwa nyingi au wakati wakiwa wako kwenye msongo  wa mawazo, hasa wakati wa ukame au ugomvi. Inafaa kufanya uchoraji wa ramani wakati usiokuwa na joto kali- mapema asubuhi au jioni. Hata hivyo, inapowezekana uchoraji wa ramani ukamilike ndani ya siku moja, kwa kuwa itakuwa usumbufu kwa mchakato kuahirishwa hadi kesho yake na ni vigumu kutunza ramani kutokana na misukosuko.





Kwa kawaida, ramani itachorwa juu ya ardhi. Hii inaweza kufanyika kwa kutumia chaki kwenye eneo lisilo laini, au na kijiti kwenye eneo la udongo lililo tambarare. Ni muhimu eneo liwe tambarare na lisiwe na mawemawe au uoto; kuwe na nafasi ya kutosha kutembeatembea na kuangalia vizuri mchoro; eneo hili lilindwe dhidi ya mifugo au watoto wanaoweza kuharibu ramani; na lihifadhiwe (dhidi ya upepo, jua, na mvua). Pia inasaidia kama sehemu hiyo ina mwonekano wa eneo hilo au sehemu ya eneo linalochorewa ramani. Washiriki wanaweza kupata usumbufu kidogo kama eneo linalochorewa ramani liko mbali kidogo kutoka kwenye makazi yao. Tembelea eneo kabla ya siku ya zoezi la uchoraji ramani ili kuhakikisha kwamba linafaa.

### Fanya mkutano wa utambulisho

Timu ya uwezeshaji iandae mkutano wa utambulisho kwa washiriki wa uchoraji wa ramani kutoka katika jamii. Mkutano huo utatumiwa kujadili kwa kina kuhusu zoezi la uchoraji wa ramani na unapaswa kufanyika siku chache kabla uchoraji wa ramani haujafanyika. Katika mkutano huu timu ya uchoraji wa ramani itafanya yafuatayo:

- Kutambulisha mchakato wa uchoraji wa ramani, kuelezea kwa nini uchoraji wa ramani una umuhimu mkubwa ndani ya kuandaa mpango wa matumizi bora ya ardhi ya kijijina kwa namna gani/wapi unafaa. Kazi ya uchoraji wa ramani itambulishwe kama sehemu ya mchakato wa muda mrefu ambao utahakikisha muendelezo wa matumizi ya upatikanaji wa rasilimali za nyanda za malisho kwa ajili ya jamii ya eneo hilo.
- Kukipa kikundi taarifa za uchoraji shirikishi wa ramani na mchakato wa utekelezaji. Kueleza ni muda gani, nguvu na rasilimali gani zinahitajika.;

- Kuthibitisha muda muafaka na mahali ambapo uchoraji wa ramani utafanyika, na kufafanua kuhusu usafiri na mipangilio ya viburudisho/vyakula;
- Kutambulisha timu ya kuwezesha uchoraji wa ramani na kuanza kujenga uhusiano na wanajamii;
- Kuangalia kufaa kwa upigaji picha na/au kupiga picha mchakato wa uchoraji ramani.



### Andaa vifaa vya uchoraji wa ramani

Hatua ya mwisho katika kujiandaa kwa ajili ya uchoraji wa ramani ni kuhakikisha kuwa vifaa vyote muhimu vinapatikana. Hivi vinajumuisha:

» Zana za kusafishia eneo, ikiwa ni pamoja na brashi ya kusafisha uchafu. Kama eneo halina kivuli, basi itakuwa vizuri kuweka turubali kwa ajili ya kivuli;

» "Kikasha cha kutunzia vifaa vya kuchorea ramani" cha vitu ambavyo vinaweza kutumiwa kupima ardhi na kuongezea vile ambavyo jamii inaweza kutumia. Hii inaweza kujumuisha vitu kama vile kamba, utepe, chaki na udongo wa rangi tofauti tofauti, kadi za rangi na kalamu, mawe ya ukubwa tofauti, na vitu vingine kama vijiti, nyasi na majani;

» Chatipindu na kalamu za rangi kwa ajili ya kunakili ramani;

» Karatasi za kuandikia na kalamu;

» Kamera kwa ajili ya kupigia picha za mchakato wa uchoraji wa ramani na ramani ya mwisho, na /au vifaa vya video.

### Chapisha orodha ya uchoraji wa ramani ya rasilimali ya ardhi ya malisho

Katika kiambatisho cha 1 ni orodha ya uchoraji wa ramani imetolewa. Hii itachapishwa na kutumiwa katika shughuli za ugani ili kuhakikisha kwamba vifaa vyote vipo na kazi zote muhimu zinafanyika.

# 2



# Ngazi ya 2
## Uwezeshaji:
## Kuchora ramani


Ngazi ya 2 inalenga uchoraji shirikishi wa ramani ya rasilimali za nyanda za malisho. Hatua zitakazofuata hapa ni:

» Hatua ya 4. Kuchora ramani ya nyanda za malisho

» Hatua ya 5. Kuongeza taarifa

» Hatua ya 6. Kamilisha ramani




UFUNGUO
MNADA/MARKET
MPAKA WA KIJIJI/VILLAGE BOUNDARIES
DIMBWI LA MAJI/PONDS
MBUGA/GRASSLAND
MAKAZI YA KUDUMU/PERMANENT SETTLEMENTS
MABOMA YA MUDA/TEMPORARY SETTLEMENTS
AGRICULTURAL ENCROACHMENTS
NJIA ZA MIFUGO WAKATI WA MASIKA
/CATTLE ROUTES (WET SEASONS)
BECKON



# Hatua ya 4

## Chora ramani ya nyanda za malisho

*Hatua ya maandalizi ikiwa imekamilika, timu ya uwezeshaji na jamii inaweza kuanza hatua ya 2- kufanya uchoraji shirikishi wa ramani ya rasilimali ya nyanda za malisho. Rasilimali muhimu zinaweza kuchorwa kwanza na taarifa nyingine kufuatia.*

### Wezesha ufunguzi wa zoezi hili na utambulisho

Shughuli hii itaanza na sherehe fupi ya ufunguzi ambayo itaakisi taratibu za mila na desturi. Muda pia utolewe kwa ajili ya ufafanuzi wa malengo na mchakato wa uchoraji wa ramani – Inaweza kutokea mshiriki akajiunga na kundi akiwa amechelewa, hivyo wanahitaji kupewa taarifa hizo. Kipindi cha utangulizi kinaweza kujumuisha:

- Kupokea ruhusa ya kufanyika kwa mkutano kutoka kwa kiongozi au viongozi wa jadi, kadri inavyofaa
- Kuitambulisha timu ya uwezeshaji wa uchoraji wa ramani
- Kuwataka washiriki kujitambulisha wenyewe
- Kueleza malengo ya zoezi na mchakato, na kuhakikisha uelewa wa pamoja wa masuala yote; na
- Kuthibitisha kwamba kila mmoja anajisikia vizuri kushiriki kwenye mkutano, pamoja na kuwepo eneo hilo na ratiba ya siku hiyo.



## Anza kuchora ramani

Mwezeshaji aiambie jamii kuanza kuchora ramani ya rasilimali za nyanda za malisho. Ni utaratibu mzuri kuanza zoezi la uchoraji ramani kwa shughuli ambayo ni rahisi sana, ili jamii zielewe mara moja nini cha kufanya. Swali rahisi na la wazi husaidia washiriki kuchukua udhibiti mara moja juu ya maudhui na yatakayokuwemo kwenye ramani: kwa mfano, "Je, unaweza kutuonyesha (kwenye ramani) sura za nchi(mazingira mbalimbali) zilizopo katika eneo lenu?" Kama jamii watapata ugumu, mwezeshaji atawasaidia kupendekeza baadhi ya sura za nchi kama vile mlima, mto, au ukingo wa msitu, kisha atahimiza ubainishaji wa sura zingine zinazohusiana na hivyo. Hii itasaidia washiriki kujifahamisha na kupima sura ya nchi kwenye eneo la ramani.

Mwanzoni washiriki wa jamii wanaweza kuhitaji kuhimizwa kutumia matawi, mawe, changarawe, majani, majivu, mkaa, au hata kinyesi cha wanyama kuwakilisha rasilimali za nyanda za malisho vikisimama badala ya vifaa vilivyopo katika "kikasha cha uchoraji wa ramani". Hata hivyo, uzoefu unaonyesha kwamba mara baada ya kuanza, mara moja watachukua udhibiti wa uchoraji wa ramani na kuwa wabunifu wa kutumia vitu vinavyopatikana katika eneo husika. Mara baada ya sura ya nchi kuchorwa, mwezeshaji atakitaka kikundi kuonyesha taarifa muhimu kwa kuoanisha na lengo la kwanza la zoezi la uchoraji wa ramani. Kwa mfano, hii inaweza kuonyesha rasilimali asili muhimu ambazo jamii imekuwa ikizitumia. Katika suala hili kikundi cha uchoraji ramani kinaweza kubainisha maeneo tofauti ya malisho, vyanzo vya maji, maeneo ya kukata majani, na maeneo ya kudumu ya kulima mazao. Kikundi kinaweza kuonyesha eneo husika na kuongeza taarifa za kina zinazofaa kwa usimamiaji wa wanyama, m.f. taarifa kama vile za wapi panapatikana malisho na aina za mimea zinazopatikana hapo, mahali ambapo udongo wa madini au chemchemi na chumvi zinapatikana, au maeneo yanahusiana na magonjwa ya wanyama. Hakikisha kwamba matumizi ya msimu ya rasilimali yanaonyeshwa. Ili kuhakikisha kwamba matumizi na watumiaji wote wa ardhi ya malisho wanawakilishwa, mwezeshaji aulize makundi tofauti, m.f, "Je, umeonyesha rasilimali ambazo wafugaji wa kike wanatumia?"

Uzoefu unaonyesha kwamba utaratibu mzuri si ule wa kuanza na mipaka inayozunguka eneo hilo (angalia Kisanduku cha 3). Kufanya hivyo kunaweza kuzuia uchoraji ramani ya rasilimali hizo na maumbile ya asili yaliyomo ndani ya mpaka huo, na rasilimali nyingine zinazotumiwa na jamii nje ya mpaka zinaweza zisitajwe au kujumuishwa. Hata hivyo, ikiwa, kikundi kinachochora kinasisitiza uchoraji wa mpaka kwanza, mwezeshaji ahakikishe kwamba kuwepo kwa mipaka hiyo hakumaanishi rasilimali zilizo nje zimeachwa.

## Weka ufunguo wa ramani pamoja na alama na rangi zinazofaa

Kukamilisha ramani ya rasilimali za nyanda za malisho, jamii inapaswa kuandaa ufunguo ambao unafafanua bayana kwa kutumia alama na rangi maumbile asili mbalimbali yaliyoonyeshwa kwenye ramani. Mwezeshaji ahakikishe kwamba wanatumia alama na rangi hizohizo kwa maumbile asili ya aina moja m.f. kwa kutumia matawi kwa viunga vya msitu na mawe kwa makazi. Anaye nakili ramani ajaribu sana kutumia alama na rangi hizohizo kwenye ramani iliyopo katika karatasi.

### Andika majadiliano yote yanayoandamana na zoezi hilo

Mchukua taarifa arekodi majadiliano yote yanayoendelea wakati ramani inachorwa. Taarifa nyingi zitatokana na orodha ya maswali yatakayosomwa na mwezeshaji, lakini ni muhimu pia kurekodi taarifa za ziada, mjadala na matakwa halisi yanayoibuka wakati wa zoezi hili. Mchukua taarifa pia ajaribu kurekodi nani anayezungumza na nani anayechora. Pale panapotokea kutoelewana, mchukua taarifa anapaswa kurekodi mitazamo hiyo tofauti, ikiwa ni pamoja na kikundi cha watumiaji ambacho kimeweka mtazamo huo. Wakati majina ya maeneo yakitajwa, anayenakili ramani na mchukua taarifa wanapaswa kujitahidi kuyarekodi kwa usahihi, lakini uhitaji wa taarifa zaidi haupaswi kumaanisha kwamba majadiliano yanayoendelea yanavurugwa. Itakuwa muhimu kusubiri hadi zoezi la uchoraji wa ramani likamilike kabla ya taarifa kama hizo kunukuliwa na taarifa zozote zinazokosekana kujazwa.





## Amua muda unaofaa kwa mapumziko na kufunga

Mwezeshaji hapaswi kuharakisha shughuli hii bali kwenda kwa kadri ya mweleko wa jamii, kuhimiza majadiliano miongoni mwa washiriki ili kufafanua mchakato wa uchoraji wa ramani. Lakini mwezeshaji anapaswa pia kuchukua tahadhari ili zoezi hili lisichukue muda mrefu mno. Kama kikundi kitaanza kuonyesha kukosa hamu na kiwango cha ushiriki kuanza kupungua, mwezeshaji asimamishe zoezi hili na ajadiliane na washiriki muda unaofaa kwa ajili ya kikundi hiki kuanza tena. Kadri uchoraji shirikishi wa ramani unavyokaribia kukamilika, mwezeshaji atahitaji pia makadirio ya muda upi unafaa kufunga. Bila shaka ramani itakamilishwa ndani ya muda wa siku moja; hata hivyo, ikiwa kutabainika kuwepo na upungufu mkubwa unaohitaji kujazwa, mwezeshaji awatake washiriki kurejea asubuhi ya siku inayofuata ili kukamilisha zoezi hili. Ramani inahitaji kulindwa ili isivurugwe wakati wa usiku.

### Kisanduku cha 3: Mambo muhimu ya kuzingatia wakati wa uchoraji wa ramani ya nyanda za malisho

*1. Uchoraji wa mipaka*

Mipaka inaweza kuzuia nafasi ya kuchora ramani. Unapoanza na mchakato wa uchoraji ramani jaribu kuepuka kuchora mipaka ya eneo linalopimwa. Hii inaweza kuzuia uaandaji wa ramani pasipo sababu za msingi na kusababisha sehemu muhimu za nchi nje ya mipaka kukosekana na kuacha kushughulikiwa. Kwa mfano, eneo la msitu au la malisho lisilotumiwa mara kwa mara na jamii linaweza lisiwepo kwenye mipaka iliyowekwa awali, na hivyo ramani yenye mipaka iliyoainishwa awali katika mchakato wa uchoraji ramani inaweza kutoa picha yenye vitu baadhi au picha ya uongo ya upatikanaji wa rasilimali, ufikiaji na utumiaji. Zaidi ya hayo, kwa kuanza na mipaka ya utawala (au mingine), mwezeshaji anaweza bila kujua kumaainisha kwamba mipaka ni muhimu zaidi.

Uchoraji wa ramani unatumiwa kama zana ya kuboresha usimamizi wa rasilimali zinazotumiwa kwa pamoja na maeneo tofauti, kwa hiyo ni muhimu kwamba mipangilio ya usimamizi wa rasilimali isipotoshwe au kukosekana katika ramani. Ni utaratibu mzuri kuanza na ramani ya rasilimali za nyanda za malisho zikiwa na rasilimali zote zilizoainishwa, kisha kuwaambia washiriki kuchora mipaka yoyote muhimu. Katika kuweka mipaka kwenye ramani, washiriki watabainisha rasilimali hizo ambazo zinaweza kuwa zinasimamiwa na kijiji kimoja na zile zinazohitaji usimamizi wa vijiji kadhaa.

*2. Uchoraji ramani ya mabadiliko ya msimu katika upatikanaji na matumizi ya rasilimali.*

Wafugaji na wawindaji-wakusanya matunda hutumia rasilimali tofauti kwa nyakati tofauti katika kipindi cha mwaka. Hii ni kwa sababu ya mambo mawili: upatikanaji wa rasilimali na usimamizi wa rasilimali hizo. Mabadiliko ya msimu ya rasilimali na matumizi yake ni taarifa muhimu na inahitaji kuonyeshwa kwenye ramani, kwa kutumia picha, alama na rangi tofauti.

Maeneo makavu ya nyanda za chini ambapo wafugaji hufanya shughuli zao yanakabiliwa na ukame mkali na misimu ya mvua. Ikiwa lengo mahsusi ni kuelewa mabadiliko ya msimu, inaweza kuwa muhimu kufanya uchoraji shirikishi wa ramani za rasilimali za nyanda za malisho ili kuelewa kikamilifu tofauti hizo.

*3. Uchoraji ramani ya uhamaji*

Uchoraji ramani ya kuonyesha uhamaji wa mifugo na watu ni kazi nyingine muhimu ya uchoraji wa ramani ya rasilimali za nyanda za malisho, lakini inaweza kuwa changamoto. Umbali unaotembewa unaweza kuwa mkubwa au mdogo, kutegemeana na msimu na hata mwaka husika. Inaweza kuwa vigumu kuonyesha taarifa zote muhimu na kiasi cha safari inayofanywa na watu pamoja na wanyama katika ramani ya rasilimali ya nyanda za malisho iliyojaa tayari, hivyo ramani tofauti ya kuonyesha uhamaji inaweza kutakiwa (hili litajadiliwa zaidi hapo chini).



# Hatua ya 5

## Ongeza Taarifa

*Ramani ya rasilimali za nyanda za malisho itakuwa chanzo cha taarifa za msingi katika mchakato wote wa usimamizi endelevu wa ardhi ya malisho. Taarifa za ziada zinazohusiana na sehemu ya anga zilipo rasilimali hizo zitahitajika kuongezwa kwenye ramani*



### Majadiliano yatakayozingatiwa na kikundi cha uchoraji ramani ili kuongeza taarifa

Kulingana na malengo ya zoezi la uchoraji wa ramani kama lilivyokubaliwa na jamii, taarifa za nyongeza na za kina zitahitajika kuongezwa kwenye ramani ya rasilimali za nyandaza malisho. Mara ramani ya msingi inapochorwa, mwezeshaji anapaswa kupitia malengo ya uchoraji wa ramani pamoja na wahusika wa uchoraji wa ramani na orodha yake ya maswali ili kikundi kiweze kuongeza taarifa za kina kwenye ramani.

### Kuchora ramani ya uhamaji na njia za mifugo

Kwa mfano, lengo moja linaweza kuwa kuelewa mwelekeo wa uhamaji (mifugo na watu) ndani na nje ya eneo hilo.

Sifa muhimu katika usimamizi wa maliasili na hivyo ndani ya Mpango wa Matumizi Bora ya Ardhi ya kijiji ni uhamaji wa mifugo (na watu) katika kutafuta maji na malisho. Hata hivyo, kama ilivyofafanuliwa awali, uchoraji ramani ya uhamaji ni mgumu na unahitaji kikundi kinachochora ramani kuuliza maswali kwa makini na kushawishi ili kupata taarifa zinazotakiwa (angalia Kisanduku cha 4).

Mahali ambapo kuna mambo mengi na mchanganyiko, kuyaonyesha yote katika ramani kunaweza kuwa kugumu kwani kunahitaji taarifa zaidi na kufanya ramani kujaa mambo mengi. Kwa hiyo, inaweza kuwa muhimu kuwa na ramani tofauti, au kwa wanaonakili ramani kuweka utokeaji wa uhamaji kwenye ramani tofauti. Njia mbadala ni kuchora njia za uhamaji/mifugo katika nakala ya ramani inayochorwa kwenye karatasi ya kunakilia, ambayo inaweza kuwekwa juu ya ramani halisi inapohitajika. Utumiaji wa taarifa za mfumo wa kijiografia (‘GIS’) baada ya ramani kuchorwa unaweza kuwa muhimu kwa ajili ya kuunganisha seti za data tofauti na ramani.

Ili kuandaa ramani tofauti ya uhamaji au kuonyesha uhamaji kwenye ramani iliyopo, orodha ya maswali kwa ajili ya mwezeshaji kuuliza inaweza kujumuisha yafuatayo:

- Huwa unasafiri kwenda wapi na mifugo ipi kwa ajili ya malisho au kuvinjari?
- Huwa unasafiri kwenda wapi na mifugo mifugo ipi kutafuta maji kwa ajili yao?
- Huwa unasafiri kwenda wapi kutafuta au kutumia maliasili nyingine na huwa ni kwa madhumuni gani?
- Huwa unafanya safari hizi kipindi gani na mara ngapi?
- Kwa nini huwa unafanya safari hizi?
- Nani huwa anafanya safari hizi?
- Huwa unarudi na rasilimali zipi kutoka katika safari hizi?
- Ni kina nani kutoka "nje" ya jamii hii ambao huwa wanasafiri kuja katika eneo hili kutumia rasilimali hizi na kwa nini?

Mchukua taarifa anapaswa kuchukua kwa uangalifu kumbukumbu za uhamaji huu na majadiliano yanayohusiana nayo.

### Kisanduku cha 4: Uchoraji wa ramani ya uhamaji


Ramani za uhamaji zinaonyesha wapi, kwa nini, na wakati gani watu na mifugo husafiri. Taarifa za uhamaji zinaweza kujumuisha:

- » Tarehe na kujirudia kwa safari;
- » Njia, umbali, na mahali wanapoenda
- » Sababu za kusafiri
- » Tofauti baina ya wanaume, wanawake, vijana wa kiume na wa kike;
- » Njia za kusafiri zinazounganishwa na kupatikana kwa rasilimali, ikiwa ni pamoja na fedha taslimu.

Ramani za uhamaji zinaweza kuchorwa kuonyesha uhamaji wa makundi tofauti ya wafugaji kutoka vijiji tofauti, au uhamaji wa kikundi kimoja. Uhamaji wa mtu binafsi au kaya unaweza kuonyeshwa pia. Njia za uhamaji zinaweza kupimwa kwa aina/spishi tofauti za wanyama, na ramani zinaweza kuonyesha pamoja na matumizi ya msimu na utoaji wa umiliki wowote au eneo la malisho, maeneo ya maji, majosho ya kuogeshea mifugo n.k.

Ramani ya uhamaji inaweza pia kuonyesha maeneo ambayo yanatembelewa mara kwa mara na kwa hiyo yanaweza kuwa na mwingiliano mkubwa na hatari ya kutumiwa kupita kiasi. Matokeo yake, hili linaweza kuhitaji usimamizi na ulinzi maalumu. Mbadala wake, ramani inaweza kuainisha maeneo ambayo hayatembelewi mara kwa mara au hata wakati mmoja na kwa hiyo kuwa na uwezekano wa kutotumika ipasavyo. Ni muhimu kutafuta sababu za uhamaji huo na kwa nini baadhi ya maeneo yanatembelewa sana kuliko mengine. Suluhisho linaweza kubainishwa kutatua matatizo yoyote kama vile matumizi makubwa, kutotumika ipasavyo, na migogoro ya rasilimali.

Inawezekana kutoa ramani ya kawaida uhamaji wa wanyama kwa ajili ya tahadhari ya mapema. Ramani hizi zinaweza kujumuisha maeneo makubwa na hata mkoa mzima. Kwa kuelewa na kufuatilia uhamaji wa wanyama, uhamaji usio wa kawaida unaweza kugundulika kama dalili ya mapema ya msongo/kuzidiwa na kwa hiyo kuwa zana ya tahadhari ya mapema katika eneo la malisho.



### Kuchora ramani ya rasilimali muhimu na/au rasilimali zinazohitaji usimamizi maalumu

Lengo la pili linaweza kuwa kuelewa hali ya rasilimali na eneo la ardhi ya malisho linalohitaji ulinzi au usimamizi maalumu katika nyanda za malisho.

Ramani ya rasilimali ya nyanda za malisho iainishe mahali na hali ya maliasili (m.f maji, maeneo ya malisho, hifadhi ya chakula cha mifugo), pamoja na eneo ambalo linahitaji hatua za usimamizi maalumu (m.f . hifadhi ya malisho ya msimu).

"Tija ya nyanda za malisho katika sehemu zenye matatizo" ni rasilimali muhimu ambayo wafugaji wanahitaji zaidi katika kuendeleza tija ya njia zao za kujipatia riziki kulingana na ufugaji wa wanyama. "Maeneo haya yenye matatizo" yanaweza kuonyeshwa kwenye ramani.

Orodha ya maswali yanayolenga kwenye maeneo ya malisho, kwa mfano, yanaweza kujumuisha yafuatayo:

- » Nini kinachofanya "eneo la malisho kuwa zuri"? Nini kinachofanya eneo la malisho kuwa "baya"? Ni eneo lipi la malisho ulilolichora kwenye ramani ambalo ni "zuri" au "baya"?
- » Nini kifanyike kuboresha eneo la malisho ambalo umelichora?
- » Ni eneo lipi la malisho lina umuhimu mkubwa kwenye mfumo wako wa uzalishaji wa mifugo?
- » Ni maeneo yapi ya malisho uliyoweza kuyafikia hapo zamani ambayo sasa huwezi kuyafikia?
- » Ni wapi kuliko na maeneo ya malisho ambayo yana uwezekano wa kusababisha mgogoro?

## Kuongeza mipaka na migawanyo ya matumizi ya ardhi

Katika Hatua ya 4, ilishauiriwa kwamba mipaka ya kijiji, au kitu kingine kinachohitaji kuzingatiwa, kisichorwe mapema katika mchakato wa uchoraji ramani. Hata hivyo, kwa lengo la kufafanua usimamizi wa mpango wa sekta ya nyanda za malisho, mpango wa pamoja wa matumizi bora ya ardhi, au cheti cha hatimiliki ya kimila kwa eneo la malisho linalochangiwa, ni muhimu kuonyesha mipaka na migawanyo iliyo muhimu kwa ulinzi na usimamizi wa eneo. Sasa ni muda unaofaa kwa mipaka ya eneo la usimamizi wa malisho na/au kijiji hicho kuchorwa kwenye ramani ya rasilimali za nyanda za malisho.

Mpaka (na kwa hakika ramani yenyewe- angalia hapo chini) utahitaji kujadiliwa na kuthibitishwa na jamii kwa mapana, serikali ya mtaa, na vikundi vilivyo jirani. Vikundi vilivyo jirani hususani vinaweza kupinga mpaka na kwa hiyo, kufuatia zoezi la uchoraji ramani (na kabla ya ramani kutumiwa kwa matumizi maalumu), mchakato wa kujadiliana na kufikia mwafaka unaweza kuhitajika ili kufikia mapatano. Inaweza kufaa kuonyesha mpaka kama mstari wenye nukta, kumaanisha kwamba kuna njia inayokatisha.




Mzozo wa mpaka ulitatuliwa huko Kisanga kwa msaada wa mradi mdogo wa utafiti uliofanywa na wanafunzi na walimu wa ITC na Chuo Kikuu cha Ardhi na Stadi za Usanifu Majengo (UCLAS- sasa Chuo Kikuu cha Ardhi), kwa kushirikiana na CARE TANZANIA (mradi wa Misitu Yetu). Mipaka ilikuwa na mizozo kwa sababu ya kutokuwepo kwa mipaka bayana, kukosekana kwa umiliki, na mazungumzo ambayo hayakutosheleza baina ya makundi yenye mzozo. Kama hatua ya kwanza ya kuelewa hali ilivyo, wanajamii walisaidiwa kuchora kielelezo cha ramani ya eneo hilo. Ili watafiti wabainishe uelekeo, alama kadhaa ziliwekwa na 'GPS'. Picha za setilaiti za 'Landsat Thematic Mapper (TM) 'zenye uonekano wa mita 30 liliachwa kusaidia katika mwonekano wa ramani.

Kuonyesha mipaka yenye mizozo kwenye ramani kunafanya eneo lenye matatizo kuonekana kwa uwazi na kusaidia kutafuta jitihada za wanakijiji wanaohusika kutatua matatizo hayo. Hakuna njia nyingine ya kutatua mzozo wa mpaka ila kwa kutumia uchoraji wa 'GPS', matokeo yanayoonekana husaidia majadiliano. Ubora na matumizi mengi ya taarifa zilizorekodiwa zikiwa muunganiko wa msaada wa dijitali binafsi ('PDA') na 'GPS' kutegemea na ujuzi na maarifa ya mwendeshaji, maarifa maalumu huhitajika kuandaa muundo sahihi ili matumizi ya zana yawe ya moja kwa moja.

Mipaka mingine na migawanyo ambayo inaweza kuonyeshwa kwenye ramani ni pamoja na mipaka ya kiutawala, migawanyo ya matumizi ya ardhi, umiliki wa ardhi ya biashara, eneo la dola; na maeneo ya udhibiti wa wanyamapori.

Anayechukua taarifa anapaswa kuandika kwa umakini majadiliano yote yanayohusu mpaka na masuala ya mgawanyo.



# Hatua ya 6

## Kamilisha ramani

*Mara timu ya uchoraji ramani na washiriki watakapokubaliana kwamba ramani shirikishi ya/za rasilimali za nyanda za malisho zitakuwa zimekamilika, kuna hatua kadhaa ambazo timu ya uchoraji ramani itapaswa kufanya ili kuhitimisha hatua hii ya mchakato mzima*

### Mwezeshaji

Mwishoni mwa zoezi la uchoraji wa ramani, mwezeshaji atapaswa kulishukuru kundi kwa ushiriki, taarifa na muda wao. Inapaswa kufafanuliwa tena kwa nini taarifa hizi ni muhimu na jinsi zitakavyotumika. Jamii inapaswa kupewa fursa ya kuuliza swali lolote watakalokuwa nalo. Mwishoni, utaratibu unapaswa kufanyika kwa ajili ya kikao kijacho, ambapo washiriki wa uchoraji wa ramani watawasilisha ramani yao ya rasiliamali za nyanda za malisho kwa jamii kubwa kwa ajili ya majadiliano na uthibitishaji (Hatua ya7).

### Mchukua wa Taarifa

Mwishoni mwa zoezi la uchoraji ramani, mchukua taarifa anapaswa kuhakikisha kwamba taarifa zimekamilika na kama hazijakamilika, atumie muda unaotakiwa pamoja na washiriki kujaza taarifa katika nafasi zilizowazi na kufafanua jina la eneo na taarifa nyingine muhimu.

### Anayenakili ramani

Mara baada ya kukamilika kwa ramani shirikishi, anayenakili ramani anapaswa kupiga picha ya ramani hiyo, kupata nakala nyingine ya ramani iliyochorwa. Itafaa kupiga picha hii akiwa juu, huku akitazama chini iliko ramani iliyochorwa (kwa mfano, kusimama juu ya gari), ili ramani yote iweze kuingia katika picha. Anayenakili ramani anapaswa kutumia ramani hii shirikishi ya rasilimali na michoro ya ugani kuweka taarifa za ramani ya mwisho katika karatasi (karatasi ya chatipindu au karatasi kubwa).



Anayenakili ramani anapaswa kuhakikisha kwamba ufunguo uliotumika katika ramani iliyopo katika karatasi ni sawa na ule au unalingana na ule uliotayarishwa na washiriki wa uchoraji ramani. Rangi ileile au inayofanana inapaswa kutumika pia.

Taarifa zifuatazo zinapaswa kutumika katika ramani shirikishi ya rasilimali za nyanda za malisho (au nyuma ya ramani):

- Tarehe ambayo ramani ilichorwa;
- Eneo ambalo ramani ilichorwa;
- Majina ya timu ya wachoraji wa ramani;
- Majina ya wanajamii walioandaa ramani hiyo;
- Kaskazini inapaswa kuonyeshwa juu ya ramani, lakini maelekezo ya ramani kama ilivyochorwa na jamii hayapaswi kubadilishwa ili kulingana na kaskazini.

Nakala za ziada za ramani ya rasilimali za nyanda za malisho zinaweza kutolewa kwa kutumia karatasi zenye ukubwa wa A3 (au A4) – hii inaweza kufanyika ama kwa kuskani na kupunguza ukubwa au kwa kunakili kwa mkono. Ramani kama hiyo inaweza kuingizwa kwa urahisi katika ripoti.

Mara ramani inayochorwa katika karatasi itakapokamilika, inapaswa kuhakikiwa na washiriki, au angalau kikundi kidogo cha washiriki, kabla ya kuwasilishwa katika jamii kubwa (katika hatua inayofuata).

Kwa kufuata orodha (Kiambatisho cha 1), hakikisha kwamba hatua zote katika mchakato wa uchoraji wa ramani zimekamilika.



# Ngazi ya 3
# Uthibitisho:
# Kuhakikisha ramani

Hatua hii inalenga kufuatilia hatua mara tu ramani shirikishi ya rasilimali za nyanda za malisho ikishatolewa. Hatua hizi ni pamoja na:

» Hatua ya 7. Washirikishe wadau

» Hatua ya 8. Andika ripoti

» Hatua ya 9. Rurudisha ramani kwa jamii


HUDUMA
ZINATOLEWA
HAPA
RAMANI YA KIJIJI CHA NGADOLO
KUONESHA NJIA ZA MIFUGO


RAMANI YA KIJIJI CHA NGABOLO KUONESHA
RASILIMALI ZA MIFUGO



# Hatua ya 7

## Washirikishe wadau

*Mara ramani ya rasilimali za nyanda ya malisho itakapokuwa imeandaliwa, ni muhimu kuhakikisha na kuthibitisha taarifa zilizokusanywa. Hii inaweza kufanyika kupitia mkutano ambapo kikundi cha watu wa uchoraji wa ramani kitawasilisha ramani yao katika jamii kubwa ikiwa ni pamoja na Halmashauri ya Kijiji kwa ajili ya kupata maoni yao, pamoja na kutumia vyanzo vingine kuhakikisha taarifa hizo (kupitia "uthibitishaji wa taarifa").*

### Andaa mkutano wa kupata maoni

Mkutano wa kupata maoni kutoka kwa jamii unapaswa kuandaliwa haraka iwezekanavyo baada ya zoezi la uchoraji wa ramani ili kuwasilisha ramani katika jamii na wadau wengine. Inafaa zaidi kwa washiriki wa uchoraji ramani wao wenyewe kufanya hili badala ya timu ya uwezeshaji wa kuchora ramani, ingawa washiriki wanaweza kuhitaji msaada kutoka kwa timu kwa ajili ya kutatua kutokubaliana. Timu inapaswa kuzingatia mgogoro au marekebisho yoyote ambayo yanapaswa kufanyika. Halmashauri ya kijiji na wajumbe wote wa kamati ya Usimamizi wa Matumizi Bora ya Ardhi ya Kijiji wanapaswa kushiriki katika mkutano huu.

Kwa ujumla, imegundulika kwamba mkutano huu husababisha baadhi ya taarifa za nyongeza na kumekuwa na kutokubaliana kwa kiwango kidogo. Hata hivyo, kama kutatokea kutokuwepo kwa usahihi kwa kiwango kikubwa kutasababisha kuongezeka kwa kutokukubaliana, inashauriwa kwamba mkutano uruhusiwe kuendelea hadi kumalizika na kwamba kikundi kidogo kikutane kusuluhisha masuala yoyote yaliyopo. Ni muhimu kwamba ramani ya mwisho ya rasilimali za nyanda za malisho iwe na uidhinishwaji mkubwa wa jamii, ikiwa ni pamoja na viongozi na watu walio wengi.

Kutatua migogoro kunaweza kuhitaji kwamba timu ya uchoraji wa ramani ishiriki katika kazi ya uhakikishaji wa taarifa (uthibitishaji wa taarifa) kusaidia kutatua tofauti za mawazo (tazama Kisanduku cha 5). Katika matukio kama hayo, jamii inaweza kuhamasishwa kuunda kamati ya kutatua migogoro itakayoshirikiana na timu ya uchoraji ramani.



### Kisanduku cha 5: Ufuatiliaji na uhakiki wa ramani

Kuna idadi kubwa ya vyanzo na njia ambazo timu ya uwezeshaji wa kuchora ramani inaweza kuhakikisha taarifa. Mchakato wa kufanya hili unaitwa "Ufuatiliaji na uhakiki" Mifano ni pamoja na:

*i) Usaili na mijadala ya vikundi lengwa*

Kamati na timu ya uchoraji wa ramani wanaweza kupanga kukutana na wanajamii wanaohusika ambao wanazitunza na kuzitumia moja kwa moja rasilimali zinazozungumziwa. Inashauriwa kwamba mikutano hii ifanyike katika eneo maalumu la ardhi yenye mgogoro.

*ii) Ukusanyaji wa taarifa katika eneo halisi*

Timu ya uwezeshaji na kamati wanaweza kuhakikisha hizo sura za uso wa dunia kwa kwenda katika eneo halisi lililopo katika ardhi kwa kulitembelea na kuona eneo lililochorewa ramani. Hili linaweza pia kufanyika kwa kutumia kifaa cha kupimia maeneo ya kijiografia ('GPS'), ambayo itaweza kutoa taarifa ambazo zinaweza kuingizwa katika zana za mfumo wa taarifa za kijiografia('GIS').

*iii) Vyombo mbalimbali vya habari: vya kusikiliza na video*

Wafugaji wengi na wasiojua kusoma na kuandika wamezoea kuwasiliana kwa mdomo. Uelewa mkubwa wa wenyeji kuhusu ardhi unashirikishwa katika muundo wa masimulizi na hekaya na huelezwa kwa macho (pamoja na vitendo). Kwa kutumia Vyombo mbalimbali vya habari (video na vya kusikiliza) wanaweza kutoa njia muhimu ya kurekodi taarifa ambazo zinaweza kuwa rahisi zaidi kwa mfumo wa uelewa wa wenyeji. Uandaaji wa video za uchoraji ramani na kanda unaweza kufanyika wakati mmoja na zoezi la uchoraji wa ramani na/au kama vipindi tofauti ambapo jamii ilirekodiwa ikifafanua kilichoingizwa katika ramani.

*iv) Ramani rasmi*

Ramani rasmi zinaweza kupatikana katika serikali za mitaa (au ya taifa) au katika ofisi ya Asasi Isiyo ya Serikali (AZISE). Hizi zinaweza kutumika kuhakiki baadhi ya vitu muhimu vya jamii kupitia tena usahihi wa jumla wa sehemu vilikowekwa. Ramani zinazoonyesha vitu kama udongo, maji, topografia na uoto wa asili zinaweza pia kutumika.



# Hatua ya 8

## Andika ripoti

*Ramani ya rasilimali za nyanda za malisho ni waraka pekee muhimu unaosimama peke yake, lakini ripoti inayoambatana nayo itatoa pia taarifa muhimu ya usuli kwa ajili ya mchakato wa kuandaa mpango wa matumizi Bora ya Ardhi ya kijiji. Ni muhimu kwa wachukuaji wa taarifa kuandika taarifa hiyo katika mchakato wa uchoraji wa ramani na mjadala unaohusiana nao haraka iwezekanavyo mara baada ya zoezi hilo.*

Ripoti ya uchoraji ramani inaweza kufuata muundo ufuatao:

| Ripoti ya uchoraji wa ramani ya nyanda za malisho | |
|---|---|
| **1** | Ukurasa wa kichwa cha habari wenye tarehe, mwandishi na taarifa za mawasiliano |
| **2** | Shukurani |
| **3** | Utangulizi |
| **4** | *Taarifa za eneo la ugani*<br>Tarehe<br>Jina la jamii<br>Eneo<br>Aina kuu za mifumo ya kujipatia kipato<br>Majina na jinsi za washiriki<br>Majina ya timu ya wachoraji wa ramani na kazi na majukumu yao |
| **5** | Malengo makuu na madogo ya zoezi la uchoraji ramani |
| **6** | *Nakala ya ramani*<br>Nakala ya kipimo cha ramani na picha ya ramani halisi iliyochorwa na washiriki |

| | | |
|---|---|---|
| **7** | *Taarifa za mijadala ambazo zimeambatishwa katika uchoraji ramani*<br>Inapotokea uchoraji wa ramani unakuwa na malengo zaidi ya moja, ni muhimu kwamba taarifa hizi ziwasilishwe, zikiakisi hoja iliyoibuliwa na washiriki. |
| **8** | *Taarifa zinazohusu migogoro*<br>Sehemu hii ya ripoti inapaswa kuweka kumbukumbu ya mgogoro wowote au kutokubaliana ambako kulitokana na zoezi la uchoraji wa ramani na jinsi migogoro hiyo ilivyotatuliwa. |
| **9** | *Taarifa kuhusu viwango vya ushiriki*<br>Sehemu fupi ya kutafakari inafaa katika zoezi la uchaguzi wa washiriki na viwango vya washiriki, ikiwa ni pamoja na wanajamii ambao walishiriki au wasumbufu |
| **10** | *Hitimisho na hatua zinazofuata*<br>Maliza ripoti ya uchoraji wa ramani kwa hitimisho lolote na hatua zinazopendekezwa kufuata, ikiwa ni pamoja na muda uliopangwa. |



# Hatua ya 9

## Rudisha ramani kwa jamii na washirikishe na wadau wengine

*Kurudisha ramani shirikishi ya rasilimali za nyanda za malisho katika jamii kwa ajili ya matumizi yao, pamoja na wadau wengine, ni muhimu.*



Ni muhimu kwamba angalau nakala tatu za ramani zenye vipimo zirudishwe kwa jamii, kwa pamoja na idadi sawa ya nakala za ripoti ya uchoraji ramani na picha zilizopigwa. Hili linaweza kufanyika kupitia kikao rasmi cha jamii pale ambapo ramani imepokelewa na viongozi wa jamii. Kama itawezekana ramani na ripoti vinapaswa kuwa katika lugha ya Kiswahili pamoja na lugha za kienyeji (kama itaonekana kuwa muhimu). Ili ramani hiyo iweze kutumika kama waraka wa kurejea, inashauriwa kwamba iwekewe jalada la plastiki ili iweze kutumika mara kwa mara katika vikao vya jamii bila kuwa na hatari ya kuharibika. Kwa madhumuni ya kuandaa mpango wa matumizi bora ya ardhi ,ni muhimu kwamba timu ya usimamizi wa mpango wa matumizi bora ya ardhi ya kijiji iwe na angalau nakala moja. Kama ikiwezekana, washiriki wa uchoraji wa ramani wanapaswa pia kupewa nakala yao.

Aidha, kufuatia ushauri wa washiriki wa uchoraji ramani na viongozi wa jamii ya wenyeji, nakala za ramani na ripoti zinaweza kutolewa kwa:

- Ofisi za serikali ya mitaa na wilaya zinaohusika na mpango wa matumizi bora ya ardhi na usimamizi wa maliasili na maendeleo ya wafugaji, ikiwa ni pamoja na timu ya Usimamizi Shirikishi wa Matumizi ya Ardhi na Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya, kwa ajili ya kuitumia katika kuandaa mpango wa matumizi bora ya ardhi ya kijiji na michakato ya mipango katika ngazi ya wilaya;
- AZISE nyingine na mashirika ya jamii za kiraia yanayofanya kazi katika eneo hilo;
- Taasisi na vyuo vikuu vya utafiti wa maeneo makame nchini.

Mara tu zoezi la uchoraji wa ramani ya rasilimali za nyanda za malisho litakapokamilika, timu ya uwezeshaji na jamii ya wenyeji wataendelea kushirikiana katika hatua zinazofuata za michakato ya kupanga mipango ya mautumizi bora ya ardhi(tazama Hatua ya 4). Ni muhimu kuendelea kukutana na jamii kila mara ili kuendeleza ushirikiano mzuri, ambao utaimarika katika shughuli za siku zijazo.

### Kisanduku cha 6: Kutambua haki ya milki ya ubunifu

Ni muhimu kwamba mashirika yaliyoshirikishwa katika uchoraji wa ramani kutambua kwamba taarifa zilizowasilishwa katika ramani ni mali ya jamii ambapo zoezi la uchoraji wa ramani limefanyika,hata kama imechorwa kama matokeo ya zoezi lililowezeshwa. Kwa hiyo, timu ya uchoraji wa ramani "haimiliki" taarifa, ramani wala nakala za ramani. Matumizi ya ramani yaliyopangwa ya siku zijazo kwa ajili ya taarifa, uratibu na utetezi yanapaswa kujadiliwa na kukubaliana na jamii. Utunzaji maalumu unapaswa kufanyika kwa kukubaliana matumizi ya ramani shirikishi za rasilimali za nyanda za malisho kwa lengo la utetezi. Kama kutakuwa na uhitaji, mikutano ya ufuatiliaji inaweza kuandaliwa pamoja na wanajamii ili kutafuta msaada wao na kuidhinishwa kwa matumizi yaliyopangwa.



# Ngazi ya 4

## Matumizi:

## Kutumia ramani


Hatua zinazopaswa kuchukuliwa katika kutumia ramani shirikishi za rasilimali za nyanda za malisho ni:

» Hatua ya 10. Mipango


» Hatua ya 11. Usimamizi

» Hatuaya 12.Ufuatiliaji na tathmini




Ramani ya Matumizi Bora ya Ardhi Kijiji cha Mongo wa Mono na Yaeda Chini
0
5
10
15
20
25
Mongo
wa
Mono
Yaeda
Eshkesh
Survey and Mapping Division,
Ministry of Lands, Tanzania, 1975
Grid: UTM Zone 36 South





# Hatua ya 10

## Mipango

*Ramani shirikishi ya rasilimali ya ardhi ya malisho ni zana ya thamani na chanzo cha taarifa kwa kupanga mipango ya matumizi bora ya ardhi na mipango mingine au michakato ya usimamizi.*

Mara hatua ya 1, 2, na 3 zitakapokuwa zimekamilika, ramani ya rasilimali ya ardhi ya malisho itakuwa tayari kutumika katika mipango, usimamizi na ufuatiliaji wa rasilimali za nyanda za malisho. Jambo la muhimu ni mtumizi yake katika kuandaa mpango wa matumizi bora ya ardhi ya kijiji kama waraka wenye taarifa za kutosha za rasilimali za nchi na usimamizi, ambavyo vinaweza kuunda msingi wa makubaliano na maamuzi kuhusu matumizi na ushirikianaji wa rasilimali na kugawanya ardhi ya kijiji katika matumizi mbalimbali ya ardhi. Inaweza pia kutumika kama msingi wa Ufuatiliaji na Tathmini.

Ili kuendeleza na kutekeleza mpango mzuri wa matumizi bora ya ardhi ya kijiji, taarifa za kina kuhusu matumizi na usimamizi wa rasilimali zilizopo zinahitajika. Ramani ya rasilimali za nyanda za malisho na ripoti inayoambatishwa nayo vinawakilisha vyanzo vinavyoonekana na vilivyoandikwa vya taarifa hizo. Hii inajumuisha taarifa zinazokwenda na wakati kuhusu yafuatayo: rasilimali ikiwa ni pamoja na rasilimali zinazotumiwa kwa kushirikiana, aina na matumizi ya ardhi, mwelekeo wa jumla wa matumizi ya ardhi, maeneo muhimu yenye wasiwasi na mgogoro, muundo wa utawala na maeneo au rasilimali ambazo zitahitaji uangalizi au ulinzi maalumu. Hata hivyo, uchoraji wa ramani ya rasilimali za nyanda za malisho ni zana mojawapo miongoni mwa nyingi ambazo zinaweza kutoa taarifa zinazofaa katika mchakato wa kuandaa mpango wa matumizi bora ya ardhi ya kijiji.

Uchoraji wa ramani ya rasilimali za nyanda za malisho unaweza pia kuwa na matumizi muhimu katika mpango wa mabadiliko ya hali ya hewa. Kuchora ramani inayoonyesha matukio tofauti tofauti ya hali ya hewa kunaweza kusaidia kutathmini na kupanga madhara yanayotarajiwa ya kuongezeka kwa mabadiliko ya joto, mabadiliko ya unyeshaji wa mvua na mabadiliko ya uoto wa asili na misimu. Hili ni eneo la kazi ambalo linaweza kufaa kuendelezwa na kupanuliwa.



Huko Duru Haitemba, Babati katika mkoa wa Manyara, uchoraji shirikishi wa ramani ya kidijitali ulitumika, kwa kusudi la kuwawezesha washiriki wa uchoraji wa ramani na jamii katika kushirikishana uelewa, kuongeza utambuzi wakati na baada ya zoezi la uchoraji wa ramani. Uchoraji ramani wa jamii na ushirikishaji wa taarifa za mfumo wa kijiografia ('GIS' & (PGIS) ulithibitishwa kuwa ni njia inayofaa kuchunguza migogoro na migawanyo yake ya muda. Kazi hii ilifanyika pamoja na mradi wa LAMP. Taarifa zilikusanywa kupitia ramani zilizochorwa kwa mkono, ukusanyaji wa taarifa halisi kwa 'GPS' na picha za satelaiti za Asta ('Aster') 2005, kutengeneza vitu vilivyopo juu ya ardhi na matumizi yake katika eneo la utafiti ili kuona migogoro katika ramani hizo. Picha za programu ya ArcGIS 9.1 na ERDAS 8.7 ilitumika kwa ajili ya uchanganuzi na uonyeshaji wa migogoro na mabadiliko katika rasilimali ya eneo la ufugaji na ugawanyaji wa picha ili kuonyesha vitu vilivyopo juu ya ardhi na matumizi yake katika eneo la utafiti.*

* C.G. Mandara (2007) Participatory GIS in Mapping Local Context of Conflicts over Pastoral Resources. A Case Study of Duru Haitemba – Babati, Tanzania. MSc thesis submitted to the International Institute for Geo-Information Science and Earth Observation, Enschede, Netherlands.

Ingawa ramani iliyochorwa kwa mkono inaweza kuwa wasilisho linalosomeka na kutumika zaidi la taarifa hii kwa ajili ya jamii za wenyeji, timu ya matumizi bora ya ardhi ya wenyeji inaweza kuhitaji taarifa itakayowasilishwa katika namna rasmi zaidi. Hii inaweza kufanikishwa kwa njia nyingi ikiwa ni pamoja na:

» Alama za msingi za ardhi zilizochorwa katika ramani zinaweza kutumika katika ukusanyaji wa taarifa kwa kutumia usomaji wa 'GPS' na kuzihamishia katika 'GIS'. Usomaji unapaswa kufanywa na wanajamii ambao walichora ramani ya mkono ili kuhakikisha kwamba alama zilizowekwa ardhini zina taarifa za kutosha. Vinginevyo, 'Google Earth'inaweza kutumika kusoma 'GPS' na jamii iliyosaidia kuonyesha alama kutoka katika ramani yao waliyoichora kwa mkono katika ramani ya 'Google Ear th' ya eneo hilohilo. Kikundi cha Tanzania cha watumia taarifa za kijiografia kijulikanacho kama 'Tanzania GIS User Group ( TZGISUG)" inawasaidia watumiaji na watu wenye shauku ya taarifa za kijiografia ('GIS') nchini. Mamlaka katika Wilaya ya Longido ikisaidiwa na Jukwaa la Maliasili Tanzania (TNRF) na Taasisi ya Kimataifa ya Mazingira na Maendeleo (IIED), wameandaa kipimo cha ramani za sura ya nchi (eneo la malisho) ya rasilimali za wafugaji na mifumo ya pamoja ya utafutaji riziki kwa wafugaji. Ramani hizi zitakuwa zikitumiwa na watendaji wa wilaya kuandaa sheria ndogo kwa ajili ya ulinzi wa usimamizi mzuri wa rasilimali muhimu za ufugaji, ili kuuongoza umma katika aina nzuri ya uwekezaji kulingana na kusaidia maendeleo yenye uthabiti wa hali ya hewa na kutatua masuala ya ushindani na utata wa kupanga matumizi ya ardhi katika viwango tofauti na kwa mamlaka tofauti. Ramani za mtazamo wa jamii na Google Earth zilitumika kuelewa na kubaini mitindo ya utafutaji wa riziki wa wenyeji. Kwa kuhusianisha ramani zilizoandaliwa na jamii pamoja na ramani za 'Google Earth', imewezekana kuandika uelewa wa wenyeji na kuonyesha katika kiwango cha kati na rahisi kueleweka na wana mipango wa serikali. Hii inawezesha mazungumzo, uelewa na heshima kubwa

kati ya wafanyakazi wa serikali na wananchi – msingi mkuu ambapo unajenga michakato shirikishi kwa ajili ya kuandaa mipango na utawala wa rasilimali kwa ajili ya maendeleo ya uthabiti wa hali ya hewa na tabia ya nchi. Ramani za ngazi ya kata za 'Google Earth' zimeunganishwa katika ramani moja pana ya wilaya na kuwasilishwa kwa ajili ya mjadala na uhalalishaji katika mfululizo wa mikutano ya jamii kuanzia katika ngazi ya kata hadi wilaya. Imehakikiwa na taarifa zaidi zimeongezwa kabla ya kutolewa kwa ramani ya mwisho na kuidhinishwa na Halmashauri nzima ya Wilaya. Katika hatua hii ramani za 'Google Earth' zimebadilishwa katika ramani za karatasi.[4]

» Taarifa kwa ajili ya ramani zilizochorwa kwa mkono zinaweza kuhamishiwa katika ramani zinazoonyesha sura ya nchi juu ya uso wa ardhi. Hii inapaswa kufanyika katika uwepo wote au baadhi ya wanajamii walioshiriki katika uchoraji ramani.. Hii inaweza bado kuhitaji ukusanyaji wa taarifa halisi za alama muhimu na mipaka kwa kutumia 'GPS'. Nchini Tanzania ramani za juu ya uso wa ardhi zinaweza kupatikana kutoka Tume ya Taifa ya Matumizi Bora ya Ardhi.

4 T. Rowley, C. Hesse, A. Harfoot, and H. Zwagastra (forthcoming) Participatory Digital Map Making Using Local Knowledge and Open Source GIS to Inform Appropriate Spatial Planning in Support of Climate Resilient Mobile Livestock Keeping in Arid Areas of Kenya and Tanzania. PLA Notes. IIED, London.

» Taarifa kwa ajili ya ramani zilizochorwa kwa mkono zinaweza kuhamishiwa katika picha za satelaiti. Hii inapaswa kufanyika wakiwepo baadhi ya wanajamii walioshiriki katika uchoraji ramani, kama sio wote. Hii inaweza bado kuhitaji ukusanyaji wa taarifa halisi za alama muhimu na mipaka kwa kutumia 'GPS'. Uamuzi wa juu wa picha za satelaiti ni gharama, japokuwa mara inapohitajika picha moja inaweza kuhusisha zaidi ya kijiji kimoja. Nchini Tanzania picha za Landsat 5 TM, Landsat 7 ETM+, na Landsat 5 TM (1994, 2001, 2008) zinapatikana. Katika mradi uliosaidiwa na Taasisi ya Jane Goodall katika Hifadhi ya Taifa ya Gombe, picha ya satelaiti ilitafsiriwa na jamii za wenyeji. Majina ya kinyeji ya milima, vijito, makazi yaliyotawanyika na sura nyingine za nchi zilikuwa zikikosekana katika taarifa zilizopo za uchoraji wa ramani. Njia ya uchoraji shirikishi wa ramani ilifanikiwa kujaribiwa na Mradi wa TACARE katika vijiji vitano vinavyopakana na hifadhi. Njia hiyo ilitumia satelaiti kurekodi mitazamo na uelewa wa wenyejiw juu ya sura ya nchi na matumizi ya ardhi na maadili. Wenyeji wana uzoefu mdogo katika usomaji wa ramani, lakini waliweza kwa urahisi kutambua sura za kijiografia katika picha ya satelaiti ya 1-m IKONOS iliyochapishwa kwa kipimo cha 1:7,000. Wanakijiji waliweza kuhusisha maeneo katika sura ya nchi na "kusafiri kwa mawazo" katika picha kuonyesha sura nyungine za ardhi. Walikuwa na uwezo wa kuonyesha mipaka kama vile miti, mawe, vijito vidogo, misitu, njia za miguu na madaraja; mashamba ya michikichi, migomba na mihogo; na maeneo ya ibada kama vile makanisa, misikiti na maeneo ya imani za kimila.



# Hatua ya 11


## Usimamizi

*Ramani ya rasilimali za nyanda za malisho na mipango ya matumizi ya ardhi itabainisha matumizi tofauti ya ardhi na rasilimali ambazo zinahitaji mifumo maalumu na hatua zake tofauti za usimamizi.*



Kama rasilimali za nyanda za malisho zitasimamiwa vizuri, zinahitaji sio tu mipango dhahiri ya usimamizi, lakini pia utekelezaji wake. Sera na sheria za Tanzania zinahamasisha usimamizi mzuri wa rasilimali zote, lakini katika baadhi ya rasilimali zinazotumika kwa kushirikiana ambazo vinginevyo zinaweza kuwa chanzo cha mgogoro. Kwa mfano, pale ambapo rasilimali zinatumika kwa kushirikiana kati ya vijiji viwili au zaidi, mpango wa sekta ya usimamizi wa maliasili unapaswa kuwekwa na kutekelezwa. Ramani inayoeleweka na yenye taarifa za kutosha za rasilimali za nyanda za malisho ni mchango muhimu katika hili.

Kuwezesha umiliki wa mpango wa usimamizi kupitia mipango ya jamii na kufanya uamuzi ni msingi wa uendelevu wa mpango wowote ambao jamii inatarajiwa kutekeleza. Kwa kutumia ramani ya rasilimali za nyanda za malisho ni njia ya wazi ya kufanikisha hili. Ramani imekuwa ikiandaliwa na kumilikiwa na jamii na hivyo taarifa hii inaweza kutumika kama msingi wa kuendeleza na kutekeleza mpango, kujadili masuala ya rasilimali na kukubaliana kuhusu shughuli za usimamizi.




# Hatua ya 12

## Ufuatiliaji na tathmini

Ramani ya rasilimali za nyanda za malisho na taarifa zinazohusiana ni msingi mzuri wa kufuatilia na kutathmini mabadiliko katika ardhi, rasilimali na matumizi na usimamizi wake. Mipango ya usimamizi wa kufuatilia wa rasilimali za nyanda za malisho kwa kutumia ramani shirikishi za rasilimali za nyanda za malisho unawezesha mameneja wa rasilimali asili kutathmini hatua za usimamizi wa madhara. Ramani za rasilimali za mwaka zinaweza kutumika kujadili maendeleo ya usimamizi na mabadiliko ya hali ya rasilimali. Ramani za ufuatiliaji wa eneo la malisho zitasaidia katika kutoa taarifa zinazohusiana na masuala mapya ya usimamizi yanayoibuka na kuhitaji kushughulikiwa katika mpango uliorekebishwa wa usimamizi.

Ufuatiliaji ni muhimu kwa rasilimali au ardhi ambazo zipo chini ya matumizi makubwa na/au yaliyopo hatarini. Ramani shirikishi za rasilimali za nyanda za malisho zinaweza kutolewa/kuboreshwa kila baada ya kipindi fulani kama mchango wa ufuatiliaji huu. Taarifa zilizozalishwa kutokana na ufuatiliaji huu za mabadiliko na mwelekeo zinapaswa kutathminiwa na kurejelewa katika mchakato wa usimamizi, ili michakato na hatua ziweze kufuatwa ili kuzingatiwa.





## Kiambatisho

Orodha ya Uchoraji wa ramani ya rasilimali za nyanda  za malisho

1

## Kuanza

### Utangulizi

- ☐ Wanachama wote wa timu  wawe wameelezwa malengo ya zoezi la uchoraji wa ramani.
- ☐ Timu ya uwezeshaji iwe imeandaa orodha ya maswali yanayotakiwa kujibiwa.
- ☐ "Kikasha cha uchoraji ramani" cha vifaa kiwepo kwa ajili ya kutumiwa na jamii.

### Timu ya uwezeshaji

- ☐ Timu iwe na angalau wajumbe watatu.
- ☐ Timu ijumuishaewanaume na wanawake.
- ☐ Wanachama wote wa timu wawe wamepata mafunzo ya uchoraji wa ramani na mbinu shirikishi.
- ☐ Timu zote ziwe zimesoma mwongozo wa uchoraji ramani.
- ☐ Majukumu ya timu yabainishwe (mwezeshaji, anayenakili ramani (mchoraji) na mchukua taarifa).
- ☐ Timu zote ziwe zinazungumza lugha ya kienyeji (kama hazizungumzi, mkalimani awepo).
- ☐ Angalau mwanachama mmoja wa timu awe anatoka katika eneo la wenyeji.

### Kuiendea jamii

- [ ] Maofisa wa serikali za mitaa wawe na taarifa na kuidhinisha shughuli na malengo.
- [ ] Wazee/viongozi wa kimila wawe na taarifa na kuidhinisha shughuli na malengo.
- [ ] Iwe imeelezwa vizuri kwa jamii kuwa ni nani ambaye timu ingependa ashiriki katika mchakato wa uchoraji wa ramani. Uchaguzi wa washiriki unapaswa kuakisi malengo ya timu na kuwa na wawakilishi wa jamii. Kikundi cha uchoraji wa ramani kitahushisha angalau watu sita.
- [ ] Utaratibu wa zoezi hilo uwe umeelezwa vizuri kwa washiriki, ikiwa ni pamoja na muda, malipo, usafiri.
- [ ] Muda na mahali pa kufanyia zoezi hilo viwe vimekubalika.

2

## Utengenezaji wa ramani

### Mchakato wa uchoraji ramani

- ☐ Timu iwe imetambulishwa kwa jamii.
- ☐ Malengo ya uchoraji wa ramani yawe yamefafanuliwa vizuri kwa jamii.
- ☐ Majadiliano yamefanyika kuhusu kile kinachopaswa kuonyeshwa katika ramani na kwa kipimo kipi.
- ☐ Uchoraji wa ramani umeanza kwa maswali rahisi, kama vile: "Ni sura zipi kuu za nchi zilizopo katika eneo hili?"
- ☐ Mpaka ulioongezwa baada ya ramani umekamilika (sio wakati wa kuanza).
- ☐ Rasilimali zote zimeingizwa katika ramani, ikiwa ni pamoja na zilizopo karibu/mbali (kulingana na malengo yako).
- ☐ Maeneo n amajina yameandikwa vizuri.
- ☐ Ufunguo wa kufafanua alama umewekwa.
- ☐ Mazungumzo yamefanyika wakati wa uchoraji wa ramani kwa kuzingatia orodha /maswali.
- ☐ Washiriki wote wamechangia katika zoezi.
- ☐ Masilahi katika zoezi yamezingatiwa na washiriki wote.
- ☐ Muda umetolewa kwa ajili ya maswali.

### Uchukuaji wa taarifa

- [ ] Taarifa za kina na zinazoeleweka ziwe zimepatikana kwa ajili ya majadiliano, ikiwa ni pamoja na maswali na majibu.
- [ ] Masuala ya malumbano, mgogoro na usahihi wa masilahi uwe umezingatiwa.
- [ ] Taarifa zote ziwe zimechapwa na nakala vimeambatishwa katika ramani ya kwenye karatasi kwa ajili ya marejeo ya siku zijazo.

### Kunakili ramani

- [ ] Jamii imepewa kibali cha kunakili ramani.
- [ ] Nakala ya ramani imefanyika katika karatasi ya chatipindu (au kubwa), kama ilivyochorwa na jamii(yaani hakuna mabadiliko katika uelekeo wa ramani au alama).
- [ ] Ufunguo wa kufafanua alama umejumuishwa katika ramani.

### Kufunga zoezi

- [ ] Washiriki wameshukuriwa.
- [ ] Umuhimu wa ramani hiyo na faida/fursa vimejadiliwa.
- [ ] Muda umetolewa kwa ajili ya maswali.
- [ ] Hatua zinazofuata zimejadiliwa na kukubaliwa.
- [ ] Utaratibu umeandaliwa kwa ajili ya mkutano ujao.

3

## Ufuatiliaji

### Kwa jamii

- [ ] Ramani zilizochorwa na wanaume na wanawake zimeshirikisha na kujadiliwa.
- [ ] Marekebisho yoyote ya muhimu katika ramani yamefanyika.
- [ ] Jamii imepewa nakala kamili ya ramani (ni vizuri zaidi iwe imejaladiwa kwa karatasi ya plastiki).

### Uandikaji wa ripoti

- [ ] Ripoti ya zoezi hilo iwe imeandikwa mara baada ya zoezi.

*Yafuatatyo yawe yamejumuishwa katika ripoti:*

- [ ] Taarifa za kina za ugani (jina la kikundi, idadi ya washiriki, eneo, jinsia, kazi);
- [ ] Malengo ya zoezi hilo;
- [ ] Nakala ya ramani inayoonekana vizuri;
- [ ] Muhtasari wa mjadala na maswali/majibu;
- [ ] Ufuatiliaji kufanyika, lini na kufanywa na nani.
- [ ] Nakala za ripoti na ramani (zenye ukubwa wa kutosha katika nakala iliyochapishwa na nakala tepe) ziwe zimetumwa ofisi kuu.

☐ Nakala za ripoti na ramani zimewekwa katika jalada kwenye ofisi ya timu ya uwezeshaji.

☐ Serikali za mitaa zimepewa nakala za ripoti na ramani



## Shukrani kwa wafadhili

Wabia wa Mradi Endelevu wa Usimamizi wa Nyanda za Malisho ('SRMP') wanawashukuru wafadhili wafuatao kwa msaada wao katika mradi:

Mwongozo huu wa ugani umechapishwa na International Land Coalition, ambao ni muungano wa kimataifa wa asasi za kiraia na mashirika mbalimbali ya kiserikali yanayofanya kazi kwa pamoja kukuza usawa katika upatikanaji na udhibiti wa ardhi kwa ajili ya wanawake na wanaume maskini,  kwa dhamira kwamba upatikanaji na usawa katika kupata na udhibiti wa ardhi unapunguza umaskini na kuchangia utambulisho wa mtu, utu na ushirikishwaji.

**Sekretariati ya International Land Coalition**

iliyopo katika Mfuko wa Kimataifa wa Maendeleo ya Kilimo ('IFAD'), Via Paolo di Dono 44, 00142–Rome, Italia, simu. +39 06 5459 2445 fax +39 06 54593445

Barua pepe: *info@landcoalition.org*, tovuti: *www.landcoalition.org*

